

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

**KIPKELION CONSTITUENCY, HELD AT KIPKELION CATHOLIC
CHURCH**

ON

JULY 11TH, 2002

**RECORDS OF THE PROCEEDINGS OF THE CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION,
PUBLIC HEARINGS, KIPKELION CONSTITUENCY,
JULY 11TH, 2002 AT KIPKELION CATHOLIC CHURCH.**

Present

Com. Pastor Zablon Ayonga - In the Chair
Com. Phoebe Asiyu
Com. Abubakar Zein Abubakar

Secretariat In Attendance

Irungu Ndirangu - Programme Officer,
Anthony Oluoch - Assistant Programme Officer
Regina Mwachi - Verbatim recorder
Caroline Langat - District Co-ordinator

C.C.C. Members

Emily Rutto - Committee Member
Patricia Maritim - Office Assistant
Anthony Rotich - C.E.P

The meeting started at 10.30 a.m. with Com. Pastor Zablon Ayonga in the chair.

Com. Pastor. Ayonga: We want to call the meeting to order. Ningelipenda wale wazee wako pale nyuma tafadhali njoo mchukue viti hapa mbele kwa maana tunataka kuanza mkutano. Kuna viti hapa, wacha wale watakuja nyuma wakae nyuma ninyi ambao mmekuja njoo mchukue viti vya mbele ili tuanze mkutano. Bwana Ndirangu hebu kuja hapa. Co-ordinator - kama tuna chairman wa council.....

Caroline Langat: Asante sana. Nadhani tutaanza mkutano, na kabla hatujaendelea nitaita mtu mmoja atuongoze kwa maombi. Bwana Charles Kibe karibu utuongoze kwa maombi.

Prayer (Charles Kibe): Mtu yeyote ana kofia tafadhali weka chini ili tuendeleo na maombi. Tuombe. Mwenyeze Mungu tunakushukuru sana kwa wakati huu tumekutana hapa. Ni mapenzi yako Mungu kwa vile umetulinda na kutuchunga kutoka kwa taabu yoyote na sasa Baba tunakurudishia asante sana kwa maana viongozi wetu ambao wamekuja kuchukua mambo yetu hapa, wamefika bila taabu. Tunakuomba kwa wananchi wote walio hapa na wengine tunawangoja, tukikutana katika kikao hiki Baba, utuongoze. Yale yote Baba tutakayo sema hapa ni yale Baba tunatafuta ya nchi yetu, ili nchi yetu iwe na makao mazuri kwa kila mtu. Na kwa hivyo Baba tungekuomba ututumie hayo, tusije tukawe na mafikira yetu sisi wenyewe, kwa maana hayo ni yale yale yanaleta taabu. Kwa hivyo tunakuomba na twakuita kwa kikao hiki, ututumie Baba wale wanaongoza mkutano huu, Baba uwe pamoja nao. Wasemaji uwe pamoja nao ili neno lolote tunalolisema hapa, liwe na faida kitika nchi hii yetu, na

katika taifa letu. Kwa hivyo tunakuita uje Baba uanze nasi hata umalize nasi ili mkutano huu tukiumaliza Baba, uwe wa furaha na tunaomba hayo katika jina la Yesu Mwokozi wetu.

Audience: Amen.

Caroline Langat: Okay asante sana. Kabla hatujaendelea tutafunguliwa mkutano na Bwana D.O. halafu atawachia Chairman, Town Council atusalimie pia. Karibu Bwana D.O.

Mebone Kitadzi: Commissioners, Chairman Town Council, Councillors, wananchi wote hamjambo? Hamjambo tena.

Audience: Hatujambo.

Mebone Kitadzi: Kitu cha kusema tu on behalf ya wananchi wa Kipkelion division na serikali, Commissioners mnakaribishwa na mjisikie kama muko nyumbani. Jambo la pili, nyinyi kama wananchi wa hapa, huu ni wakati wenu ambao mnataka mtoe maoni yenu, muwe free, msikue na uoga. Kila mtu useme kile kitu wewe mwenyewe unaona. Sitaongea mengi sana kwa sababu tunataka tuanze mapema, na nafikiri nitakaribisha Chairman, Town Council anene halafu tuendele. Okay asante.

Chairman: Macommissioner, Macouncillors wako hapa, wazee na wakina mama hamjambo?

Audience: Hatujambo.

Chairman Town Council: Mimi ninafikiri siku ya leo sisi watu wa Kipkelion ni siku kubwa sana. Maana tuko na wageni wanaleta mambo ya Katiba. Na mimi nafikiria tumefurahi sana kukuwa leo hapa Kipkelion. Na nyinyi wageni, karibuni halafu nyingi mtasikia yetu yale tutasema leo. Mimi nafikiri watu wa Kipkelion ni kitu kimoja. Kile kitu tutaongea hapa, wewe usikuwe na wasiwasi, sema haki hakuna pahali pengine utapelekwa. Hapa ni nyumbani na tutasema kile kitu tunataka. Usiongee kama wewe unaregesha mguu, hakuna kitu kingine wewe utaulizwa leo, lakini ile haki yako wewe uliza leo. Mimi ninafikiri tutakaa na hawa Macommissioner watachukua mambo yetu, na hawataweka kwa cupboard, watachukua kusema watu wa Kipkelion wamesema wanataka hii, asante sana.

Caroline Langat: Okay asante sana. Kabla hatujaendelea ningependa kuwatambulisha wote ambao tumekuja nao. Kwa majina ninaitwa Caroline Langat, mimi ni District Co-ordinator, katika hii district yetu ya Kericho. Tuko pia na member mmoja wa constituency committee ambaye atasema jina lake. Karibu.

Emily Rutto: Jina langu ni Emily Rutto. Committee Member, Kipkelion.

Caroline Langat: Okay asante. Nitarudisha microphone kwa Commissioners ambao wataongoza mkutano. Tuko pia na Assistant wangu ambaye anaitwa Patricia Maritim, ako upande ule wa registration ndiye ana-register wageni wanapoingia. Asanteni.

Com. Pastor. Ayonga: “Change tugul”. Sasa leo sisi tuko hapa Kipkelion, tuko Commissioner watatu, nitawapa nafasi wawasalimu. Lakini kabla hawajawasalimu, nataka nirudie yale ambayo D.O. na Chairman wa Town Council amesema. Leo ni siku yenu, siku ya namna ya pekee ambayo tumekuja hapa, si kuulizwa maswali-siku ya maswali mlikuwa mnatuuliza wakati wa civic education. Leo tumekuja mtupe maoni, si kwamba hii habari sasa ambayo nimesema muende muangalie leo. Leo sio sisi tunaenda kuangalia, ni wewe umeshaangalia unatuambia kwa kitu hiki, ninataka hivi na vile na vile. Na wengine pengine mnakuwa mkifikiri D.O. akiwemo, pengine Chief yuko, na nani yupo, nikisema hivi tukitoka jioni nitachukuliwa juu juu. Hakuna habari ya mtu yeyote kubebwa juu juu, tuna blanketi kubwa ambayo ni ya uwezo ambayo imetolewa ya kufunika kila mmoja. Mambo ambayo utasema hapa, yataheshimiwa jinsi yalivyo kwa maana tumekuita uyaseme, na uyaseme jinsi yalivyo.

Na pia, tumetaka hapa mjue kwamba hatukuja mkutano wa siasa. Tumekuja mkutano wa kutoa maoni, ninyi mko kama watu ambao wako kortini. Watu wakiwa kortini wanasikiza, mpaka ameulizwa aseme. Kwa hivyo tunataka ukimya ule, tumetaka heshima ile, tuheshimiane katika mkutano huu. Na, nitawaambia baadaye jinsi ambavyo tutafanya. Lakini kabla ya kuwaambia, nataka mjue kwamba tunawafanyi kazi wa ofisi yetu ambao wako hapa. Tunayo programme officer-Ndirangu uko wapi? Ni yule nyuma. Mkimuona mmuone kama mtu ambaye ni mfanyikazi wa Commission, ndiye anayeongoza mambo yetu ya kikazi. Halafu tunaye mama Regina, ambaye huyo ambaye ameinua mkono pande hii, ana kazi ya kunasa maneno yenu kwa kanda. Tuna hicho kimashini ambacho kinanasa kila neno unalosema. Kwa hivyo tutakuja kukuambia unataja jina lako kwanza, “mimi ni fulani fulani, na maoni yangu ni haya na yale”.

Hatukuja hapa leo mtuambie Wazungu walipokuja hapa, hii reli ilipopita hapa, jambo hili na lile lifanyika-hayo yote tulishasoma kwa shule. Tunataka mtuambie mambo mnayotaka; hatukuja hapa kwa history, tumekuja hapa kwa present. Mambo yaliyoko, na jinsi umetaka yafanywe wewe binafsi. Na wale ambao mko hapa, hatutaki mtu anaposema, na wewe unanza kusema, “la si hivyo, au ingekuwa hivi na vile”. La. Tunataka heshima kwa kila mmoja wenu. Ikiwa anasema vibaya, hayo ni maoni yake, we ngoja mpaka wakati wako utakapofika. Na kama jambo limesemwa na fulani na ndilo ulilokuwa unafikiria kusema, afadhali wakati unapoitwa ni kusema “ninazingatia yale ambayo fulani aliyasema, sina mengine mapya, ni yale yale”. Kuliko kurudia rudia na neno ni lile moja. Sasa, kabla sijasema mengine, hebu Commissioners wawasalimu. Kwanza nitaanzia na mama Bi. Asiyu, ili awasalimie.

Com. Asiyu: Asante sana Pastor Commissioner Ayonga kwa kunipa nafasi ya kuwasalimia watu wa Kipkelion, habari za asubuhi nyinyi nyote? Tumefurahi sana maana tumekaribishwa na nyinyi, pamoja na D.O. wenu na Chairman wenu. Na ninavyoona, mkutano wetu wa leo utakuwa wa mhimu na wa maana kwa maana watu wameanza kuingia kwa wingi. Nataka tu kuwakumbusha kwamba tunajenga mji mpya safari hii. Na kujenga huo mji mpya, ninyi ndio mtatuletea ile miti ya kujenga,

yale majani ya kuweka juu ya hiyo paa ya nyumba na vile vyombo vyote vitakaa kwa hiyo nyumba. Kwa maana hii nyumba tunaishi sasa, yaani hii Katiba ya leo, ilitengenezwa kule ulaya. Ijapokuwa imerekebishwa mara thelathini na nane, wakati umefika sasa ambao sisi wenyewe kabisa Wanakenya Waafrika tutajenga Katiba mpya. Na sio sisi Macommissioner tutajenga, kwanza sisi Macommissioner hatuko na maoni hata kidogo, vile Chairman wetu amesema. Maoni yenu ndio yatajenga Katiba mpya, na hiyo ni kitu cha muhimu ninataka mfikirie sana.

Kwa hivyo, mkifika kutueleza, mtueleze mambo ya muhimu na ya maana, ambayo yatasaidia kubadilisha maisha ya watu wa Kenya, ili pengine waendeleo kuishi vizuri zaidi ya vile tumeishi miaka hiyo mingine. Katiba ambayo italinda vijukuu vyenu hata kwa miaka hamsini, mia moja ijayo kama Katiba za nchi zingine zimefanya. Na mkumbuke jambo la maana sana ni kwamba, Makatiba nyingi za Africa au nchi ingine, zinarekebishwa wakati wa vita, wakati wa shida, wakati ule ambao nchi imeharibika. Sisi-mimi ninafikiri ni Mungu alifanya mpango huu-tunaandika Katiba wakati kuna shwari, na tumpe Mungu asante na pia tumpe President Moi asante, kwa maana ma President wengi, wakiwa bado wako kwa power, hawafanyi mambo kama haya huyu amefanya.

Sisi hatuzungumzii serikali lakini tunasema ukweli. Kwa serikali ya sasa kukubali na Bunge kupitisha kwamba Katiba mpya ya Kenya iandikwe. Na watu wa Kenya ambao walipigania sana sana kutafuta Katiba mpya. Kwa miaka kumi, watu wa Kenya wamekuwa wakiuliza Katiba mpya iandikwe, Bunge imepitisha Mzee ameweka sahihi na ninaona kila mtu anatupatia nguvu na support ya kuandika Katiba kamili, kuikamilisha na kupeleka report yetu kule mbele ambako, mimi ninajua mumeelezwa vile mpango wa repoti yetu utakavyokuwa tukishapeana kwa kamati ile kuu ya watu wa Kenya, ambao watakaa wajadiliane warekebishe halafu ndio Act itengenezwe ambayo itapelekwa Bunge, Wabunge wapitishie, halafu sasa iwe kamili ni Katiba mpya ya nchi mpya ya Kenya. Kwa hivyo ninawashukuru sana kwa kufika leo na kushukuru pia watu wetu ambao tumekuja nao, tumezunguka Kenya mzima tumefanya kazi ngumu kweli kusikiliza, kuwauliza maswali na pia kusaidiana nanyi ili mambo yenu na mapendekezo yenu-kila mmoja iingizwe kwa computer zetu kama imeandikwa au umezungumza-hakuna jambo hata moja litapotea vile Mzee ameeleza hapo mbele. Asanteni tunawakaribisha na tunafurahi kwa vile mmeingia na twajua kwamba sisi wote tutafanya kazi kama ndugu na hii Katiba ifanye tuwe marafiki zaidi Kenya, na tuishi kwa mapenzi zaidi ya vile hata tumeishi hapo mbele. Vile hata mliona mzee alikuwa akisema jana usiku. Asanteni sana Mungu awabariki.

Com. Pastor. Ayonga: Asante Bi Asiyu, sasa hebu Commissioner Bwana Abubakar Zein awasalimie.

Com. Zein Abubakar: Habari ya asubuhi?

Audience: Njema.

Com. Zein Abubakar: Mstahiki mwenyekiti wa baraza, Bwana D.O. viongozi mbali mbali na wananchi waheshimiwa mliofika hapa, mimi nina mambo mawili tu; la kwanza, ni kuwashukuru kwa kufika hapa na la pili ni kusema kwamba nimeshajitayarisha

vizuri kuwasikiliza maneno yenu, kwa sababu wazee wakishasema maneno, mimi kazi yangu ni kukubali, kuafiki na kusema tuendelee hivyo. Asanteni.

Com. Pastor. Ayonga: Kabla sijaanza, nimetaka kuwajulisheni mmoja wetu wa ofisi, kijana ambaye anaandika kama machine.

Hii ni sehemu ambayo anataka muelewe kabisa, mtakapoona nimekaa hivi ninasikiza au huyo ndugu yangu anasikiza au mama anasikiza handiki, mnaanza kufikiri, “na haya maneno yetu tunasema, mbona tunaona hawaandiki?” Yule mama atakuwa akinasa maneno kwa kanda, hata ukikooa, kikohozi chako kitakuwa katika record yetu. Utaambiwa, “wewe mzee unakaa na maneno na siku hii si ulikohoa, nani anakohoa kama hivyo?” Halafu, kuna kijana hapa ambaye anaitwa Oluoch-Oluoch inua mkono, - Oluoch ndiye huyo rangi mbili au rangi tatu, sasa naona ni tatu: nyeupe, blue, nyekundu. Oluoch huyu, anaandika kama chepreta. Yeye atakuwa anaandika kabisa kabisa, na yule mama atakuwa ananasa na sisi hapa tutasikiza wakati mwingine mtaona tunaandika-lakini cha muhimu kuliko vyote, ni kwamba hakuna mtu hapa hata mmoja ambaye atatoa maoni yake, yakapotea. Hakuna cha hiyo. Sasa ninataka kuwaambia taratibu jinsi ambavyo tutafanya. Nimekumbuka mimi mwenyewe kwambam - niliwaambia mimi ni nani? Mimi ni Pastor Zablon Ayonga, ni Commissioner na nitakuwa Mwenyekiti katika kikao hiki.

Sasa, ninataka mtege masikio vizuri sana kwa maana tunaenda kuanza. Mumekuja hapa ili mtoe maoni. Kuna wengine ambao mumekuja kutoa maoni ambayo mmeandika tayari, umepanga huko nyumbani, umeandika, umeandika. Nitakuambia jinsi utatoa maoni yako. Unaweza kuchagua kuleta hayo maoni ambayo umeandika.....hebu Bwana Ndirangu usimame, huyo-mbona Ndirangu usije hapa watu wasije wakapoteza maoni yao ambayo yameandikwa wakampa mtu mwingine. Unajua, Kenya ya sasa ina mambo mengi. Mtu atakuja kuwa hapa tu anakuja anapokea maoni yetu, jioni tukikuuliza yako wapi, unasema hukuona. Huyu ndiye - ikiwa umeandika, utampelekea, mnaona hiyo file, hiyo file tupu ambayo tumeleta kama sanduku la kuenda kupigia kura? Hiyo ni ya Kipkelion. Na ukisha maliza kutoa maoni yako, utampelekea hayo maandishi ili aweke kule, ayafungie katika hilo li-folder hilo la chuma hilo. Na pia utahitajika uweke sahihi katika kitabu kwamba umetoa maneno yaliyoandikwa au umekuwa ukisema maneno, bila maandishi. Kwa hivyo huyu ni mtu wa maana sana, na kila yeyote ambaye atatoa maoni hapa leo, lazima umalizie kwenda kwake. Utasikia nikikwambia, enda kule, tutakuelekeza kila wakati tukiona unataka kuenda njia ingine. Basi asante sana Bwana Ndirangu.

Kitu kingine katika huyu anayetoa maoni ya maandishi. Hata saa hizi, unaweza kuenda kwake, bila ya kungojea na kumpa maoni yako, kwa maana umeandika. Au unaweza kungojea ili katika hayo maoni yako-ngoja kidogo msikie-ili katika hayo maoni yako, kama una neno fulani unataka kuliwekea mkazo, una nafasi ya kufanya hivyo. Unaweza kuja na maoni yako, ukasema maoni yangu haya makubwa yaliyomo, moja ni hili, pili ni lile, tatu ni hili. Basi ukaenda ukampa maoni yako hayo maandishi, ukajiandikisha, atakuuliza maswali moja mawili, kama ilivyo kawaida. Halafu unaweza kutoka uende nyumbani, uende kujenga taifa kwa njia moja au ingine, au unaweza kukaa hapa, ukisikiza wengine wanasema nini. Kwa hivyo kukaa hapa si jela, ukufungiwa kwamba, wewe utakuja kutoka hapa wakati sisi tumetoka. Una uhuru wa kutoka, una uhuru pia wa kukaa. Tumelewana? Sasa, namna ya pili ya kutoa maoni, ni yule mtu ambaye huko kwake nyumbani amefikiri, amefikiri na

anataka kuja hapa sasa kusema. “nitasema hili, nitasema lile, nitasema lile” na ukisha maliza, utakwenda kwa yule Bwana Ndirangu ujiandikishe kwa maana tumenasa maneno yako.

Kwa hivyo, katika wasemaji wote hawa wawili, tuna timing-dakika ambazo mtafanya. Nataka muangalie kila mmoja ageuze kichwa aangalie nyuma. Mnaona watu ni wachache au viti vimejaa? Hall yetu hii mpya ambaye haijafunguliwa kirasmi, ninaona imejaa. Kwa hivyo, hebu tufikirie wengine; umekuja hapa kutoa maoni na fulani pia ametaka atoe maoni. Usije ukajifikiria ni wewe tu ndiye Kipkelion constituency. Hawa wote wamekuja kutoa maoni. Kwa hivyo ninaposema, tumekupa dakika tano, ni hizo tano tu. Nikikwambia dakika zako zimekwisha, ninatazamia utatatii. Sababu gani ninakukatisha? Ni kwa maana ninataka fulani na fulani pia apate nafasi. Ama si hivyo? Kwa hivyo, usije ukaniambia maneno yangu niliyo nayo ni muhimu zaidi”. Kila mmoja amekuja hapa na neno ambalo litakuwa muhimu kwake zaidi, lakini ili kila mmoja apate nafasi, lazima tutii.

Sasa, sehemu ingine, ni lugha gani tutatumia kwa kutoa maoni? Bila shaka umejitayarisha kutoka kwako nyumbani, pengine maandishi yako umeandika kwa Kingereza na unataka utoe maoni yako kwa Kingereza. Kwa hivyo, utayatoa kwa Kingereza. Mwingine amekuja na maoni, na ametaka ayatoe kwa Kiswahili, utayatoa kwa Kiswahili. Mwingine amekuja hapa na anaona hawezi Kingereza, hawezi Kiswahili, anataka atumie lugha ya mama – Kipsigis; ikiwa huwezi Kiswahili, huwezi Kingereza, tutakupa mkalimani hapa, ambaye atakutafsiria. Lakini kumbuka hivi, mkalimani kama una dakika tano, ni kana kwamba mko watu wawili mnagawana dakika tano, atakula mbili na nusu na wewe mbili na nusu. Kwa hivyo, tafadhali kama unajua Kiswahili, usije ukaseme, “sarufi yangu si nzuri ambayo inaweza kuongea Kiswahili”. Ongea Kiswahili ikupatie dakika zako tano, lakini ikiwa ni lazima huwezi, tutakupa mkalimani.

Neno jingine. Tutampa kila mtu dakika tano tukianzia. Lakini jinsi watu wanavyozidi na saa zinazidi kuenda, nitakata kutoka tano mpaka tatu, kwa nini? Ili kila mtu at least akienda nyumbani naye awe amesema kitu.

Jambo jingine, kurudia rudia jambo moja jambo moja. Kama mtu amesema maneno uliyotokea nayo nyumbani ukaja, na umesikia yamesemwa, ni heri hata usimame hapa na kusema “yangu yamesemwa mimi ni fulani fulani, na maneno ambayo niliyotaka kusema, tayari yamesemwa”. Na tutakushukuru kwa hayo.

Nimekumbuka kitu kimoja. Kuna kile kijitabu ambacho tuliwatumia-mzee inua hicho kijitabu juu. Mnakiona hicho kijitabu? Hicho kijitabu si textbook ambayo tuliwatumia, na sisi leo tuwe kama walimu ambao tunakuja tunasema, “sasa fungua pagi fulani tuanze masomo ya siku ya leo”. Hicho kijitabu kilikuwa tu changamoto kwenu. Umeshakisoma, umefikiria, leo hatutaki mtu aje hapa asimame na kusema. “Swali la kwanza katika hii, jibu ni hili” Kama tungekuwa tumekuja hapa kwa kuja kufanya hivyo, ni mtu mmoja tu ambaye angesimama hapa, atupe majibu na tena kusingekuweko na haja yetu kuja hapa. Tunesema watu wa Kipkelion tunataka mtutumie majibu kwa kile kitabu tulicho watumia-si ingekuwa namna hivyo? Kwa hivyo yeyote asiye akasimama hapa kutusomea kitabu chetu. Ni sisi tulikiandika, sisi tunataka maoni ambayo kijitabu hicho kimekuchanganya mawazo, halafu ukafikiria mambo fulani fulani. Na hiyo isitoshe, tunataka mawazo yako pia, juu ya yale ambayo hatukuandika.

Tumeelewana?

Sasa mlipokuja mmejiandikisha katika karatasi ya namna hii, na kama kuna wengine hapa ambao mmekuja na hamkujiandikisha, tafadhali kule nyuma, muende mjiandikishe. Katika hii karatasi ndio nitakayotumia kama muongozo wangu wa siku ya leo. Nitaanza na mtu ambaye alijiandikisha kwanza. Namba moja, nitafuata fuata, kwa maana hiyo ndiyo ingekuwa haki. Lakini haki hii, inaweza pia kubadilishwa, kama mtu mwingine anaweza kuwa amekuja hapa lakini yeye ni mgonjwa, kama ni mgonjwa, nikiambiwa kuna mtu mgonjwa hapa, nitamuita kwanza aje atoe maoni yake. Kama kutakuja mzee sana hapa ambaye hawezi kukaa muda mrefu, nitamuita aje ingawa amekuja nyuma, atoe maoni. Kama kuna mama, mama mja mzito, nitampa nafasi aongee arudi nyumbani. Kama kuna mtoto wa shule, ambaye amekuja atoe maoni ndipo arudi darasani, nitampa nafasi atoe maoni yake arudi shuleni. Au, kama kuna mtu ana jambo la muhimu sana na jambo hilo lake tunaweza kulisema kwamba ni la muhimu, ninaweza kumpa nafasi pia atoe maoni kabla ya wengine. Bila ya hayo, nitafuata orodha hii jinsi ambavyo nimeipata. Kama mtu ana jambo lolote ingawa limesemwa na anataka aweke mkazo fulani, anaweza kusema hayo yamesemwa lakini, ninaweza uzito fulani fulani, hiyo inakubalika kabisa. Kuna yeyote ana swali kwa yale ambayo nimesema ambayo hakuelewa vizuri? Mzee una swali gani?

Speaker: Hamuwezi kurudi hapa kesho kwa wale ambao hawakuweza kufika hapa leo?

Com. Pastor. Ayonga: La, hatuwezi kurudi hapa kesho. Kama kuna mtu ambaye atakuwa amepitiwa na kikao hiki, anaweza kututumia memoranda yake ofisi yetu huko Nairobi, through your co-ordinator au, kesho tutakuwa Belgut. Kama una uwezo wa kufika Belgut, kwa yule ambaye hakupata nafasi hii, anaweza kufika Belgut au Bomet, au Konoin au Sotik, au Molo au Rongai. Hapo pote tumetapakaa kwingi-Commission nzima iko hapa. Tuko pahali pote sio sisi tu. Tuna vikundi nane ambavyo sasa viko katika district hii na zile zingine, kwa hivyo tunaweza patikana au, unaweza kuweka vitu vyako kwa posta, tuma huko Nairobi au kama unaenda Nairobi, KENCOM House, 2nd floor, kabla ya tarehe kumi na tano. Baada ya hapo hatutachukua maoni. Sasa yale mliotupa, ndio tunaketi tunachambua chambua. Swali jingine-hilo litakuwa la mwisho tusije tuwe ni siku ya maswali.

Speaker: Sijui kama tungeanza na wale waheshimiwa ili wananchi tuingie.

Com. Pastor. Ayonga: Hapana, hapana. Nimekuambia tuna taratibu ambayo tunafuata hapa. Na tena, kama kuna mtu aliye na jambo fulani fulani lile atatuambia kupitia kwa co-ordinator-wapi co-ordinator-kama mtu anajambo anaweza kupitia kwake. Huyu dada ndiye co-ordinator wa district hii. Kwa hivyo kama una jambo, unaweza kupitia kwake yeye atanjulisha kuna jambo fulani fulani.

Speaker: Yangu sio swali, hii microphone inayotumika na wale watakuja kuzungumza, ni kuwa sisi tunapenda kama tunazungumza, tunaangalia jukua.....(inaudible)

Audience: (inaudible)

Com. Pastor. Ayonga: Hebu tusije tukaweka maneno mengine magumu. Unajua, kama umeenda kortini, utaangalia kule ambako judge yuko. Na ninyi ambao mmekuja, mmekuja kuwapa nani maoni? Sisi, kwa hivyo sisi ndio tunataka utuangelie.

Speaker: Naweza kusema jambo?

Com. Pastor. Ayonga: Hebu ngoja kidogo Commissioner Zein ana neno.

Com. Zein Abubakar: Nasema aje ndugu yangu-ikiwa ndugu yangu-nasema wewe uliyeyuliza swali, nasema hivi; ikiwa wewe hutalala leo usiku, kwa kuzungumza ukielekea huku, zamu yako ikifika, geuza ile microphone utuangelie sisi. Sawa, zamu yako ikifika geuza ile microphone utuangelie sisi tu.

Com. Pastor. Ayonga: Kwa maana-ngoja kidogo na mama ana neno.

Com. Phoebe Asiyo: Ninajua mara kwa mara tunapeana heshima kwa viongozi wetu, na tumewapatia heshima Bwana D.O. na Bwana Chairman wameongea, lakini pia kumekuja swala au ombi ili viongozi waliotambuliwa na watu wapewe nafasi. Na Pastor amesema kweli kama wanaongoza vikundi fulani, watapewa nafasi waongee. Hiyo itakuwa ni njia nzuri kama nyinyi mtakubaliana na maoni ya hawa watu. Asante.

Com. Pastor. Ayonga: Kwa hivyo, hebu tukomeshe sasa yale yote na wacha gari moshi hiyo ipite. Sasa ninataka kukitambua kikao hiki, kama kikao cha Commission na tumeanza kazi yetu sasa kama kikao. Hayo yalikuwa maelezo lakini sasa kikao hiki tumekifungua hapa Kipkelion kirasmi. Na tunaanza kazi yetu. Asante. Na hata kama ulikuja bila ya kutazamia kusema neno, na umekuja kusikiza, hii record yetu tunachukua hata wale ambao tunaita waliokuja tu kuona. Kujiandika-wale mmekaa juu ya mawe, mnaweza kuenda kule kujiandikisha. Kujiandikisha kalamu ni yetu, karatasi ni yetu, jina lako tu ndio tunataka kwa maana umekuja kwa kikao na umesikiliza ingawa hutasema kitu. Pia, baadaye ukigeuza mawazo ukasikia changa moto imeingia, basi tunaweza kukuita ukasema kitu. Asante. Tunaanza sasa. Mtu wa kwanza kujiandikisha leo, anaitwa Ezekiel Lang'at. Ninapoita ningalipenda mnafanya haraka kidogo ili tu-save time. Na ambavyo Ezekiel Lang'at unayo memorandum, ningalipenda ukisamama hapo, sema majina yako kamili jinsi yalivyo, na pia utupe maneno makubwa makubwa ya hiyo memorandum yako. Usitusomee kwa maana ofisini tuna wasomi, hii tutaenda kusoma.

Ezekiel Lang'at: Thank you very much our Commissioners. I am Ezekiel Lang'at from Lesirwa location. I have the views here from members of my location. Let us start with the Local Authority being the most basic level of government, we hold the opinion that Mayors and Chairmen of Councils, the chairman of Council that is, should be elected directly by the members. We

also have the qualification that should be there for the mayor or the chairman of Council. Commissioners, we are saying that the chairmen of Council and the Mayors should have a minimum qualification of diploma in any field-it doesn't matter the field but they should have a minimum qualification of diploma that is, and they should have good ethical values. We also have in our local area, multi-national tea farms, namely the Brookebond, we have African Highlands produce, we have Kaisugu. There should be save ways provided for these estates.

Remember our Commissioners, if those tea estates were not there, maybe our piece of land would have been larger in the acreage. That is what I am trying to say. We also have the forests like Londiani forest for example, that forest is there because we gave our land to the government, so that they have that forest in that place. We also have the Kenya Pipeline, we also have Kenya railways, we are paving way for these two companies. Now if we take for example the amount of fuel that is being transported in the Kenya Pipeline for example, at the end of the year or each year we are saying that, the amount of profits they are receiving is very large. So us as the members of this place, because we paved way for this Kenya Pipeline Corporation, we have Kenya Railways, we also provide safe custody for this Kenya Pipeline for example-suppose now we had people coming to raid and then they take their fuel, we will be held responsible for that. Now what I am saying is this; because we are paving way for these two companies, we should get something small from these companies.

Now, there is another thing which I am seeing also. Let's come to employment for example. Now as pertains tea estates, we should be given a larger percentage, us as members because we gave out that land for that tea estate to be there. We also have this Kenya Pipeline. Our members or our people from this area should be employed in that field. We also have the issue of remuneration of Councillors. We are seeing that, since the Councillors are Assistant MPs, we are seeing that they hold a very big position-they are assisting the MPs. So, we are saying that a Commission should be formed, that is the Local Authority Commission, to look into the remuneration of Councillors so that they should be given enough salaries. That is what I am trying to say. Our Members of Parliament are getting a huge salary. So we are saying that since the Councillors are assisting them, they should be given also a large salary so that they do their work well.

We also have this issue of registering parties. At present we are seeing that, I can come with my people and we register a party. Now that is not enough, we see that I may come with a register of 50,000 members from all the eight provinces of Kenya which makes the party look national an not tribal. But we also have enterprising Kenyans-people who form parties for sale. What I am saying is this; these people-there should be some measures which are put in place, so that I don't come registering parties every other time and then I wait for a Mr. Nyachae to come for example and then I sell my party to that person, I run very quickly to the registration office I register another party. That is not good.

We also have social amenities for example the stadiums. We also watch football in this place. We also play football. I don't see why we have stadiums in Nairobi, for example, we have a lot of stadiums - we have three or four. We don't have any in this place. So we are seeing that the government should provide those stadiums in each and every constituency for example, we

should have a stadium, because we also watch football, we enjoy playing football and all those.

Interjection (Com. Pastor. Ayonga): You've made your point. Any other? Your five minutes are over, just say the last thing.

Ezekiel Lang'at: There is also one thing as pertains the number of seats in Parliament. We are seeing that not everyone is considered in the Parliament, we have the disabled for example, we have people who are handicapped. We have students, they are not represented in the House. We are saying that the government should provide seats for these people. That is, we should have an MP who is there for the sake of the handicapped or the disabled. We should have also MPs for children in school, we should also have MPs for religious groups or the Kenyans living abroad, or the military or armed forces. Thank you.

Com. Pastor. Ayonga: Thank you. We have a question for you. From time to time, you are going to find us asking a person questions. We ask a question as a matter of clarity, so no problem.

Com. Zein Abubakar: Ezekiel, you have proposed that Councillors should have their salaries and benefits increased and the reason you give for that increment is that because MPs have huge salaries, therefore, Councillors should also have huge salaries. We have received a lot submissions from Kenyans, saying that infact, you should reduce MP's salaries, doctors and others, so it will be - because MPs have huge salaries, everyone else should get a huge salary. What you should tell me, do they need that increase as Councillors, what they are doing, the work they are doing do they need an increase?

Ezekiel Lang'at: Yes, the Councillors need an increase. As I said earlier, they are assistant MPs, that is what we are seeing, because an MP is the overall person for the constituency, and then in a constituency we have several wards for example.

Com. Zein Abubakar: Now, Ezekiel, they are not supposed to be assistant MPs. They play different roles. Members of Parliament make law for the nation in Parliament. Councillors serve the Local Authority in that area. They are not supposed to be assisting the MPs.

Ezekiel Lang'at: Now, as we are saying in our place that is for example in our constituency here in Kipkelion, we are seeing that the Councillors are working hand in hand with the MPs for the development of our constituency that is.

Com. Zein Abubakar: Yes it is fine, they are not the assistant of the MPs.

Ezekiel Lang'at: But they are assisting the MP. I don't see why you are.....

Interjection (Com. Asiyo): I have another question for you. Would you rather justify this increase of salary by giving more

responsibilities to the Local Authorities? Because, I cannot see any other justification if you don't give them more responsibilities.

Ezekiel Lang'at: Now, in my memorandum here I have a few things as pertains Local Authority. Thank you.

Com. Pastor. Ayonga: Before you go, you said Kenya Pipeline passes through Kipkelion and it carries a lot of oil. And then you said the railway also passes through here - and we heard an engine going by and you want something small because it passes through here. Now this railway line is ours; ours in the sense it is for Kenyan and it has to pass somewhere. Now, I want you to start thinking from Mombasa up to Busia, if all these people who railways pass through there, want something small, what will remain for this railway line? I want also you to think of the roads that we have, all the way from Mombasa to Busia, all the way from North Eastern going down to Tanzania, everybody being paid tax, because it passes through here and this is Kenya and all the tea big farms people to be paid. I thought, perhaps, the most thing you would say, you would like to see that the people of those places takes procedure in say tea farming area, that they should involve people of those areas-I mean giving them some of this unskilled jobs rather than 'importing' people from elsewhere.

Ezekiel Lang'at: That is one of the things I said, I said.....

Com. Pastor. Ayonga: But with the Kenya Pipeline what can you do?

Ezekiel Lang'at: We have the security men in the Kenya Pipeline.

Com. Pastor. Ayonga: And from all tribes from Mombasa up to here, those people will feel even the locomotive - they have all been.....

Com. Zein Abubakar: If I can just add Ezekiel. You know, first of all Kenya Railways making losses for the past 15 years.

Ezekiel Lang'at: It is the problem of Kenya Railways.

Com. Zein Abubakar: Wait wait, - it is public - it is your company. Secondly, if you ask a company like Kenya Railways to pay that kind of charge, what they will do, they will pass on the cost to those who will use the railway now. It means passengers will pay more. It means if you want to put your agricultural products on that train be it tea or coffee, whatever it is, you will pay more. So in the end you will pay more yourself.

Ezekiel Lang'at: Now what I am seeing is that there is bad management with the Kenya Railways. That is why we are not getting that money.

Com. Asiyu: Address the management of Kenya Railways.

Com. Pastor. Ayonga: Lastly-this is for the safety of everyone of us here - when you give your views, don't mention names. We are not dealing with people's names, we are dealing with issues. You see? So, we shouldn't be mentioning anybody's name. You may like him, you may not like him. But, deal with an issue. Is that clear to everybody? So please don't speak about names. Thank you. You go give that memorandum, it has become our property now and whatever you have written we are going to read. Next person is Charles Kibe. Mzee kwenda hapo utoe maoni yako. Una dakika tano.

Charles Kibe: Asante sana Commissioner wetu. Neno langu linahusu matibabu, hospitals. Ningetaka kuuliza serikali yetu, Katiba, iondoe malipo. Mtu yeyote akienda kwa hospital ni kuingia tu na kupewa dawa maana yake, tunaona watu wetu wengi wanakaa nyumbani kwa kuogopa ataulizwa senti kidogo.

Com. Pastor. Ayonga: Mzee umeshasema point, watu wapewe matibabu free, bila malipo, hiyo umetuambia point enda pointi ingine.

Charles Kibe: Pointi ingine, ni ya elimu. Katika skuli zetu tunasikia amri moja imetoka kwa Bunge ya kwamba watoto wasipigwe viboko. Maoni yangu ni mswada huu kurekebishwa, kwa maana watoto tunaona wanaharibika, hawaogopi kwa maana hawapigwi.

Com. Pastor. Ayonga: Point unayotaka kusema ni kwamba, watoto wachapwe kama wanakosa. Hayo ndiyo maoni. Halafu pointi ingine.

Charles Kibe: Sina ingine.

Com. Pastor. Ayonga: Asante sana Mzee. Uende kule nyuma ujiandikishe. Na tafadhali msipige makofi, hizo ni pointi za mzee Charles Kibe, wewe ngojea wakati wako. Mwingine ni Elisha Soi, Mzee nawe utoe maoni yako.

Elisha Soi: Maoni yangu, hata Bibilia yenyewe iko na Katiba. Maana yake, ukisikia Kumbu kumbu la torati ninakumbuka maneno ambayo yaliandikwa zamani. Kwa hivyo kitu mimi ninataka kusema ambacho uleta amani katika ulimwengu ama kwa dunia, ni Bibilia yenyewe inavyosema lazima kila mahali pawe na mpaka. Hata kwa nyumba ya mwenyewe kuna mpaka. Kuna mpaka wa mwanamke na mwanaume na watoto. Hata kiti ambacho kiko ndani ya nyumba kiko na mpaka. Kwa hivyo, mimi mwenyewe ninaona, mpaka wa kila mtu kila taifa iwe nayo maana Bibilia yenyewe - kumbukumbu la torati thelathini na mbili na fungu la saba mpaka nane. Inasema, "Kumbuka siku za zamani, uliza baba yako, uliza wazee wako ambao wanaweza kuwaonyesha jinsi Mungu alivyoweka mpaka kwa kila taifa na kila watu ambao wanaweka mpaka yao, maana dunia ilikuwa

inazungumza lugha moja na Mungu alitawanya lugha halafu kila mtu akapewa mpaka wake”.

Ya pili, mimi ninasema makao yetu ambayo tunayo, lazima serikali ikumbuke sana kuna watu ambao wanakaa makao mawili ama tatu. Anaweza kukaa hapa ama huko na akiua mtu anatoroka kwao. Inatakakiwa mtu kama ni mwenyeji wa hapa awe wa hapa. Na kujulikana kweli akiua mtu iwe kuwe na mlango wake hapa au hakuna mlango, ambao unaweza kulipa mtu huyo. Maana desturi yetu ya Kalenjin, nikiua mtu wa fulani, tatalipa na mlango wetu, kusema sasa huyu tumeua. Lazima tukumbuke, sasa mlango wetu tunaita na kulipa huyo mtu. Lakini kuna watu wengine wanakaa wakiua mtu wanatoroka. Kwa hivyo kama.....

Interjection (Com. Pastor. Ayonga): Sasa unatakaje Mzee? Unatakaje hao watu ambao wanatoroka, tuwafanyeje, maoni yako ni nini?

Elisha Soi: Maoni yangu, yule mtu ambaye ana miguu miwili, atoroke aende kwake. Yule ambaye anakaa hapa akae kabisa kama ni mwenyeji. Wasiwe na wasi wasi kukimbia pande hii na hii. Akiwa namna hiyo italeta kifo kila mara kwa watu kuuana. Nataka mtu kama anakaa hapa wakuwe ni nani huyu, wewe ni mtu ambaye ni wa mlango gani katika nchi yetu hapa, maana kwetu lazima mtu ashikwe kama mimi ni fulani, ashike huyo mtu na awe mtu wangu, na akifanya makosa, unajua tatalipa na mlango wango.

Interjection (Com. Pastor. Ayonga): Asante na ingine pointi ingine.

Elisha Soi: Pointi ingine ambayo ninaweza kusema, ni kama nimesema mambo ya mpaka, na nimesema mambo hii ya kufanya namna hiyo. Mtu wa kuuu mtu na kutoroka. Cha pili, mtu tena kama mtu yuko hapa, akiwa ameshakuwa mtu wa hapa, tunaona tena anaweza piga kura tukiwa kwa kura hapa, anawezapiga Kisumu na yeye ni mtu wa hapa awezi kubaliwa na watu wa hapa. Nataka mtu ambaye yuko hapa, anapigia mtu wa upande huu, iwe alifuata sheria ya upande huu. Yeye mwenyewe amekuwa hapa anafanya hivo, unaona mtu wa hapa, kuna mtu wa kwetu kama mama sasa wewe unakumbuka huko kwa mama hapana kumbuka kwetu hapa.

Com. Pastor. Ayonga: Asante. Na pointi ingine.

Elisha Soi: Ni hiyo tu hayo ndio mambo yangu.

Com. Pastor. Ayonga: Asante sana Mzee, na asante kwa kutumia neno la Mungu, Mungu ndiye ana Katiba iliyo kamili na watu wakimuheshimu Mungu, wataheshimu hata Katiba ya nchi yetu. Hebu kwa hayo Mzee, uende kule ujiandikishe. Asante sana. Mzee mwingine John Kahindi, nafasi ni yako Mzee.

John Kahindi: Mimi sina mengi ya kuongea, isipokuwa tu nitatoa maoni yangu. Mimi niko na maoni manne. Maoni ya kwanza, majimbo hatutaki, ni kwa sababu majimbo inatawanya watu kutoelewana na watakuwa wakikosana milele, hiyo ni ya kwanza. Ya pili, wale watu watateuliwa kupiga kura, maoni yangu ni kura ihesabiwe hapo ambapo inapigiwa, na ihesabiwe hapo hapo kwa sababu kule kutoka nje inachukuliwa inapotea na haiwezi kujulikana ilipigwa ngapi na ni mtu mgani alichukua. Maoni ya tatu, Kipkelion kuna watu wa mchanganyiko na tunaongea lugha ya mchanganyiko. Maoni yangu, ingekuwa kama kuna mchanganyiko Kipkelion na mahali pengine kama kunaishi watu wa mchanganyiko, hata utawala uwe wa mchanganyiko, isiwe ya upande mmoja. Kumaliza neno la nne, mtu ambaye anateuliwa na Rais au Mbunge kama nominated member, mtu huyu hawezi kusaidia wananchi kwenda tu anafuata yule aliyemchagua. Maoni yangu ni hayo.

Com. Pastor. Ayonga: Asante sana Mzee. Mzee unaweza kuenda kule ukajiandikisha. Emily Ruto.

Emily Ruto: Asante sana Commissioner. Mimi ni Emily Ruto nikichangia kwa upande wa land ownership. Kwa upande wa land ownership, kwa mandishi yangu ningeonelea niseme land mbeleni ilikuwa ya mzee na kwa maoni yangu nimeonelea shamba iwe ya mama na mzee na watoto. Sikusema watoto aina gani, watoto kwa jumla, wasichana na vijana kwa vile mashamba siku hizi zimekuwa shida sana.

Upande wa inheritance. Tunataka equality, kwa upande wa girls and boys kwa masomo na kwa vile hapa kwetu masomo ya wasichana iko chini sana. Vijana - msichana akifanya mtihani darasa la nane na msichana na mvulana wapite, kijana mvulana ataenda na msichana atabaki. Sasa equality kwa education. Upande wa inheritance kwa upande wa widows wale mabwana zao wameaga, unaona kuna mambo ya kifamilia. Bibi kama huyo aonekeni kama kitu lakini anaweza kunyanganywa mali. Sasa inatakikana sheria ambayo inaweza kulinda watoto na huyo mama. Yangu sikuwa nayo nyingi ninayo in written.

Com. Pastor. Ayonga: Asante mama kwa maoni yako. Ila ni kuuliza kaswali kadogo ambako sikuelewa vizuri. Umesema land ownership iwe kwa baba, mama na watoto, yaani title deed, unataka hiyo title deed iandikwe majina ya hao wote au baba na mama?

Emily Ruto: Baba na mama/children ikiwezekana.

Com. Pastor. Ayonga: Na hao children, majina yao yaandikwe au iwe children - muungano.

Emily Ruto: Muungano.

Com. Pastor. Ayonga: Okay. Thank you.

Emily Ruto: Asante.

Com. Pastor. Ayonga: Utupelekee hiyo memorandum kule na ujiandikishe. Richard Langat. Richard ufupishe muda wako kama, mtindo ndio huo tunafuata.

Richard Langat: Asante sana. Yangu nimeandika kwa Kiingereza. Yangu nimeyatangulisha, na utangulishi ni kama ifuatayo. “We the people of united federal Republic of Kenya, enact this Constitution for the benefit of all united Kenyans”. Ya pili, nimeonelea kwamba, the current Parliament should be given less powers to amend any laws in Kenya. Ya tatu, ni vyama vya kisiasa. Vyama hivi ningependelea vipunguzwe viwe viwili na serikali iwape fedha. Ya nne, serikali ya mitaa, serikali hii yaani Local Government, Mayors and Council Chairmen should be elected directly by the people. Pili, Local Authority should be given full powers to come up with its own operation, leaving alone central government with its own operation. All elected members of Local Authority shall have to meet minimum education qualification of form four certificate and above. Ya tano, ni land and property. The land owners of a given land, should own his or her land and property fully not giving any chance to the state or government and Local Authority the power to control the use of land except with the concept of the owner.

Ya mwisho ni muundo wa serikali, formation of the government. Kenya should adopt federal system of government, yaani majimbo to give people more opportunities within the government or region where they stay. Provincial Administration boundaries which were there, before or immediately after independence should be brought back to its operation. Ningependelea serikali iwe kama hivi; kuwe na Rais yaani President as Head of State na iwe ceremonial. Prime Minister, head of the government business, President, Head of Defence, District Prime Minister, head of finance, we should also bear in mind that there were boundaries after independence and we had a Prime Minister before, who was Jomo Kenyatta. Regional.....

Interjection (Com. Pastor. Ayonga): Sema, hiyo ni ya mwisho.

Richard Langat: Sasawa asante sana.

Com. Pastor. Ayonga: Asante. Kuna maswali mawili.

Com. Zein Abubakar: Umependelea ya kwamba mtu atakayesimamia Local Government awe na minimum qualification ya O-level, sasa kulingana na sera ya sasa ya elimu - uhitaji kupita mtihani unaweza kuenda darasani au private candidate. Ukakaa ukaandika jina lako kwenye ile mtihani tu, ukakaa, hatu ukafeili flat O-level, bado utapata certificate inasema wewe ulimaliza O-level, hiyo ndio maana yako wewe?

Richard Langat: Yaani awe form four na qualified.

Com. Zein Abubakar: Qualified maana yake ni nini? Ndio tunataka kujua wewe wataka pass, grade gani, maanake hata

ukaandika jina tu utapata certificate inasema alihudhuria mtihani - huyo mtu.

Richard Langat: Bora tu amefika form four na kuendelea. Hayo ni maoni yangu.

Com. Zein Abubakar: Hiyo ndio nilikuwa ninataka kujua.

Com. Pastor. Ayonga: Hayo ni maoni yake.

Com. Asiyu: Kwa mwanzo ulituambia habari ya preamble na ukaongea habari ya federal nation of Kenya. Sawa sawa nilisikia vizuri?

Richard Langat: United federal of Kenya.

Com. Asiyu: Ndio ninataka kujua, hiyo system ya federal, mpango wako juu yake ni nini, ninataka utueleze tujue.

Richard Langat: Kwa maoni yangu ninaonelea kwamba, provinces iwe na jimbo, yaani kila province iwe na jimbo na kila province iteuwe wanaowakilisha hapo kwa hiyo jimbo.

Com. Asiyu: Na mkubwa wa hiyo jimbo ni nani?

Richard Langat: Iwe ni Governor.

Com. Asiyu: Ni governor, na P.C. saa hiyo kazi yake iko wapi?

Richard Langat: Saa hiyo P.C. ninaonelea hatakuwa na kazi saa hiyo.

Com. Asiyu: Kwa hiyo yeye atakuwa governor.

Richard Langat: Aa aondolewe na watu wachague. Na system of Administration yote itaenda nafikiria.

Com. Asiyu: Okay asante.

Com. Pastor. Ayonga: Enda ujiandikishe na hiyo makaratasi utuwachie.

Com. Asiyu: Hiyo ni mali yetu sasa.

Com. Pastor. Ayonga: Joshua Rono. Stephen Kosgei yuko? Awe karibu baada ya Joshua Rono.

Joshua Rono: My name is Joshua Rono from Kisabo sublocation, Kipkelion constituency. In the preamble for the Constitution of Kenya, I would like the Constitution to have its prime objective being the equitable development and distribution of natural and human resources, together with the opportunities of utilizing such resources by the citizens of the country. Also, it should be aimed at achieving national unity, tactism and pride by all citizens.

Supremacy of the Constitution: It is expected that the Constitution shall be supreme, thereby superceding any other law of the land. Amendment of the Constitution should be such that, Parliament can amend by having a majority of 65% majority votes, but only after an approval by a special Constitution Commission and an approval by a referendum.

Shadrack Koros: We have a memorandum to represent, but actually I should touch the main points. I am Shadrack Koros, Town Clerk Kipkelion town Council. I will only touch on issues which touches on Local Government, which is Local Council. Our proposal is that Local Authorities should have their own system in the structure, organization of government, to address shortcoming of their varied personal problems of law government Act Cap 265 of the laws of Kenya. Local Authority should be autonomous, providing local democratic accountable government for locals besides their task to promote economic, social, cultural, political development for the communities. Local Authorities should provide grounds for protection, defence, efficient utilization of land resources and all other local resources. Local Authorities should be based on a council level, which shall be the highest political authority within the area of jurisdiction. With legislative and executive powers.

We are also proposing that the Mayors and the Chairmen of the council should be elected directly by the citizens and they should not actually have wards. There should be a direct election and whoever will the chairman or the mayor should not have a ward - all the wards in the council should cover his administrative powers. Also we are proposing that Local Authority should have a service commission called Local Authority Service Commission, which will actually cover for the terms and condition of service of remuneration of Councillors and staff.

On the question of nomination, we are saying that nomination should only cater for the special persons or actually should be reserved for the disabled, for the youth and women. So we are proposing that women should be - of the nominated members of the council or Members of Parliament 50% of the nomination should go to the disabled or the handicapped. We are saying 50% of the nomination, should cater for the women, another 50% of the nomination, should cater for the youth and the 3% of the nomination, should cater for the disabled. We also prefer ten percent to cater for the professionals within that area. We give them 50% and we are also saying that whoever will be nominated, will be nominated by a body. For example, if you want a nominated woman the women should nominate not the minister for Local government or the President. The women should give out or should elect and give out such and such a person to be nominated by the minister and actually the proposal should come from the group. If it is women, the women should propose and not the minister of Local government or the President. If it is the youth, the same thing, even the special groups - the professionals. The professionals should elect their own and give out for nomination.

We are also touching on the issue of...

Com. Pastor. Ayonga: Clerk, kama umemaliza kwa maana tutaenda kusoma, nadhani ungesema pointi ya mwisho.

Shadrack Koros: We are also touching on the land issue or the property rights or property over land. We are saying, all the land should be managed by the local authorities and whatever comes out of the natural resources, should be shared at the ratio of 50 – 40%. The central government should take 50%, the Local Government should take 40% to manage, so that they can

actually provide service.

Com. Pastor. Ayonga: And another 10% goes where?

Shadrack Koros: We are saying 60% goes to the central government. 40% should remain at the Local level which is the local council, to provide for services to the people within that local authority. Thank you Sir.

Com. Pastor. Ayonga: Unaweza kwenda kule nyuma ujiandikishe huko. Sasa chairman huwezi kukataa?

Cllr. Chumo: Kwa jina ni Councillor Chumo, chairman wa Kipkelion town council. Pointi yangu ya kwanza kabisa ni majimbo. Tunataka majimbo kwa maana central government, tunataka ipunduliwe kutoka central government, mali yote ije kwa council. Vile zamani ilikuwa, mali yote inabaki kwa council, inatengeneza mabarabara, mashule, afya ya watu kama hosipitali - ilikuwa wakati huo pesa zote iko kwa council. Sasa kila kitu kilienda central government tukawachwa tu vile watu wanasema hii ni council, Macouncillor wako na pesa na council haina chochote. Council hakuna chochote, mshahara wa Councillor ni 7,000/=

Com. Pastor. Ayonga: Niliwaambia msipige makofi. Wakati mwingine chairman atawafurahisha huko. Lakini kwa leo sisi tunataka tu maneno ya kushika.

Cllr. Chumo: Kwa hivyo, tukaona kama hii nyumba sasa, tunajenga kutoka chini mpaka kwa mabati kule roofing. Sisi hatuwezi kupindua roofing iangalie chini halafu chini iangalie juu. Tunataka mali yote itoke central government mpaka kwa mwananchi hapa. Kwa hivyo, hakuna kitu ingine watu wa Kipkelion wataongea kusema tunataka kitu fulani, kitu tunataka kabisa, ni majimbo halafu tuchunge nayo mali yetu na tuchunge nayo mahindi yetu na kila kitu na maziwa yetu jimbo inatosha. Tunataka jimbo. Maneno mingi ya kwenda mpaka Mombasa na kurudi, ni jimbo tunataka.

Pointi ingine ni vile tunaona kama vile mahosipitali, imelegea sana lakini kama pesa yote ya central government kuja kwa mwananchi hapa chini, hata malaria inasumbua sisi haitasumbua tena. Sitaki kuweka mengi, hiyo ni mambo tunataka hata wananchi wote wanakaa chini hapa, ile kitu tunataka ndio hiyo.

Com. Pastor. Ayonga: Ngoja, Ngoja mbona unakuwa na haraka sana.

Com. Asiyu: Nilitaka kujua mzee, hii jimbo itaongozwa na nani? Na itakuwa kwa provincial au kwa district, na ni nani atakuwa kiongozi wake.

Cllr. Chumo: Itakuwa kwa provincial.

Com. Asiyo: Na mkuu wa jimbo ni nani?

Cllr. Chumo: Atakuwa Governor.

Com. Pastor. Ayonga: Tena ngoja tu - basi kama hawana swali - wacha nikuulize swali jingine. Je unatosheka na provinces tulizonazo kwa wakati huu au tukipata serikali ya majimbo itakuwa lazima tena tuanze kuweka boundaries za majimbo ambayo yatafaa kwa wakati tuna serikali ya majimbo?

Cllr. Chumo: Hiyo lazima tutakuwa na boundary.

Com. Pastor. Ayonga: Tutakuwa na boundary. Umeanza kufikiria kama tukiwa na boundary, umesha gawa hiyo boundaries kwa kichwa yako peke yako?

Cllr. Chumo: Bado lakini si watu watakaa chini tuweke boundary. Na tena boundary zinajulikana kama Rift Valley kuna boundary yao.

Com. Pastor. Ayonga: Ndio, lakini kuna sehemu zingine nafikiri Rift Valley ni kubwa zaidi, pengine ingegawanywa iwe boundary moja na nusu. I mean jimbo moja na nusu.

Cllr. Chumo: Haiwezi kuwa jimbo moja na nusu.

Com. Pastor. Ayonga: Au jimbo mbili.

Cllr. Chumo: Itakuwa jimbo moja au watu watakaa chini.

Com. Pastor. Ayonga: Hiyo ni ya baadaye lakini kwenda weka kidole huko tujue kwamba Chairman alikuweco hapa.

Cllr. Chumo: Asante.

Com. Pastor. Ayonga: Ningalipenda tena kurudi njia ingine, kuna mama yeyote hapa ambaye alijiandisha, alitaka kutoa maoni ambaye ajaitwa? Kuna mama? Unajua sisi - kuna mama, mama si usimame? Kumbe sasa mama ni wanne. Tunataka wamama waende kupika, ingawa mlisikia watoto wanasema wasifanye kazi, wamana kuja muende muwapikie, hebu msonge hapa, wewe yule ulikuwa wa kwanza, ufuatwe na huyu nguo nyekundu, tena wale wengine mmekeki tu. Nataka hawa wamama waje hapa ili tuwape nafasi, kazi yao ni nyingi. Naona wengine nikiwaita wanaenda nyuma ile njia ingine, basi hawa ambao wamejitolea - mama sema majina yako na dakika ni mbili tu tafadhali.

Jedida Cheruiyot: Majina yangu, mimi naitwa Jedida Cheruiyot. Ninaisha Momoniot. Maoni yangu ni kama haya, masomo ya wasichana, wazazi walazimishwe kusomesha wasichana mpaka kiwango cha form four. Mali igawanywe kulingana na watoto wote, wawe wasichana ama wawe wanaume. Ningetaka tena mama hata yeye awe na mali yake, wakiwa na mzee, mama awe na mali yake mzee mali yake na wawe na mali ya pamoja.

Com. Pastor. Ayonga: Tafadhali hayo ni maoni ya mama, ninyi mngoje nafasi yenu itakapofika, kila mtu ni chake. Endelea mama.

Jedida Cheruiyot: Ningetaka tena, mashamba serikali yetu ya Kenya ione ya kwamba, kila mtu ako na sehemu yake kidogo.

Com. Pastor. Ayonga: Mama yake bwana yake?

Jedida Cheruiyot: Watu wote wa Kenya. Inginge ambayo ningetaka kusema ni ya kwamba, watoto, ningetaka kurudia mambo ya watoto niseme, watoto waelimishwe hata kama wazazi wametengana. Watoto lazima waelimishwe na wazazi wote wawili.

Com. Pastor. Ayonga: Ngoja kidogo kabla ujatoka. Mama, sikujua kama tulikuelewa vibaya ama ni lugha ilienda namna ingine au kama ulivyosema ndivyo ilivyo; haya maneno unasema bwana awe na mali yake na bibi awe na mali yake, au umesema mali ambayo iko katika kwa nyumba yenu, iwe yenu nyote wawili, ni lipi ulilosema?

Jedida Cheruiyot: Nimesema mali iwe ya mama, baba na watoto.

Com. Pastor. Ayonga: Oo wote pamoja.

Jedida Cheruiyot: Wote wawe na mali yote iwe joint.

Com. Pastor. Ayonga: Kwa hivyo wanaume, ninadhani hata ninyi mlikuwa mmeelewa vibaya, mama anasema mali iliyoko katika mji au katika boma, ni ya bwana, ni ya bibi na watoto wao - joint. Asante mama uende ujiandikishe huko. Mama mwingine kuja hapa, sema majina yako, naona unamakaratasi mengi tunataka tu utuambie pointi zilizoko hapo ndani na utupe makaratasi tuende kusoma. Dakika mbili tu.

Hariet Macharia: Asante. Mimi ninitwa Hariet Macharia kutoka Londiani. Ninasimama hapa on behalf of CMEWAK. CMEWAK maana yake ni Country Micro Enterprises Women Association of Kenya. Hawa wamama ndio wamenituma na pointi zao, proposals zao, wakaniambia nilete hapa mbele ya Commissioners. Wako na mambo mengi, ya kwanza ni kuhusu citizenship, na wako na pointi tano, of which sitaweza kusoma zote lakini ningesema, the Constitution should be reviewed to

entark a profession that will allow and provide everyone equal rights. To be automatic beneficiaries of the law. The second point is basic rights, I can only read one point: the Constitution should be reviewed to provide protection and security, health care, water, shelter, employment. It should also provide food by encouraging marketing of farm produce through proper policies.

Rights of vulnerable groups: I can only read one from there, the Constitution should be reviewed to give room and enable the handicapped person to participate equally with all Kenyan citizens on building the nation without discrimination.

Political parties and legislature and judiciary: women should be given an upper hand during their campaign rallies by being provided with security. Women or NGOs should be given a seat in Parliament or allocated a representative through nomination.

The electoral system: we have about six points on that. There should be a provision in the Constitution that dues on monitoring the candidate expenditure, to know how much the individual constant has spent on his campaign.

Interjection (Com. Pastor. Ayonga): Sasa mama sema la mwisho. Kwa maana haya yote tutaenda kusoma.

Hariet Macharia: Iko sasa land and property rights. A couple should be instructed to register their properties in their both names. The title deed should be registered and all names must appear in the document. Thank you.

Com. Pastor. Ayonga: Asante sana mama. Unaweza kuenda kule utupatie hiyo document, ujiandikishe. Mama mwingine, sema majina yako na tuambie makubwa tu ya document yako.

Petronilla Lelei: I am Petronilla Lelei.

Com. Pastor. Ayonga: Songa karibu, unasonga mbali sana.

Petronilla Lelei: I am Petronilla Lelei. I am Petronilla Lelei. I am here on behalf of Kipkelion women. Here, tuko na machache, women's critical areas of concern in the Constitution. In the bill of rights, our proposal is this; enshrine equal access of resource and equality before the law to men and women, boys and girls. In consideration of gender, race, religion, ways of life, etc.

Guarantee security and equal protection by the law to men and women. Recognize the(inaudible) groups that constitute Kenya in all aspects of life. Women rights must be guaranteed under the bill of rights.

Women participation in the legislator, local authorities, governance and decision making. Our proposal number one in our

proposal;

- 1) Separation of power of the various organs of the state, so that each organ is autonomous and self governed.
- 2) Devolution of power in all government structures to ensure Local Authorities.
- 3) Local communities participate - women will have easy access to leadership position if this happens and she has to take place in democratic to give a chance to the women and men of Kenya to participate fairly in decision making and debating on national issues.
- 4) Eliminate all form of discrimination on the basis of sex in recruitment, appointment and training in the discipline force and all other institutions of governance. Every presidential aspirant should have a running mate or V.P who is of opposite gender.

Interjection (Com. Pastor. Ayonga): Sasa mama hiyo sisi tutaenda kusoma. Sema pointi ya mwisho.

Petronilla Lelei: Pointi ya mwisho, nitasema machache tu, ya children's rights. Sasa, our proposition is, Constitution should have a clear uniform, definition of the child as any person below the age of 18 years. Recognize general human experience of non discrimination on the base of age, sex, language, look or colour, religion, opinion can apply to the child rights. Guarantee civil rights and liberty to the female and male child.

Com. Pastor. Ayonga: Asante mama. Sasa utupe maandishi kule na ujiandikishe. Kuna mama mwingine, huyo ndiye mama wa mwisho, sasa baada ya hiyo nitaanza kutafuta wazee, kwa maana sitaki wazee wakakaa hapa siku nzima ninataka waende kuona ile ng'ombe walifungia wapi. Vijana ndio tutamaliza nao mwisho.

Rael Koech: Asante sana. Jina langu ni Rael Koech. Na maneno ya Katiba vile mimi ninasema, mimi ninasema kulingana na watoto wasichana wale wako kwa shule na vijana. Sababu ni hii; watoto wale wako nyumbani wamekuwa wengi sana. Watoto wanazaa na hawajui baba yao ako wapi. Sasa tunataka mtoto kama anazaa ama kama anashika mimba, nataka tujue mwenye mimba, nataka kujua kama hachukui huyo msichana amuo, achukue huyo mtoto wake, aende awalishie, aende amusomeshe - hilo ni jukumu lake.

Interjection (Com. Pastor. Ayonga): Lakini mama, atachukua je na kwanza umesema watoto wamezaa watoto hawawajui baba yao? Sasa nani atawachukua kama hajui?

Rael Koech: Mwenye alikuwa amemuweka mimba.

Com. Pastor. Ayonga: Okey, endelea.

Rael Koech: Tena wakati wa elections, kama mnataka wamama waende elections au kuwaandika kazi, waende kwa kazi,

sasa wengine ni kama wanaenda kama wanachukua kura kwa nini watu wasema mama si kitu. Tunataka wamama tena waende wapate elimu. Kama ni assistant hata mama ni assistant chief.

Com. Pastor. Ayonga: Asante sana mama. Ya mwisho?

Rael Koech: Ya mwisho, kama mama anawachana na bwana yake na kuenda, saa zingine anaenda kufanya kazi, anaenda kupata mali, ananunua shamba. Wakati wa mwisho, hiyo mali ninataka watoto wake peke yao wagawiwe, sitaki mtu mwingine agawigwe.

Com. Pastor. Ayonga: Mama umemaliza?

Rael Koech: Bado.

Com. Pastor. Ayonga: Katika hiyo maneno ya shamba ndio ujamaliza au ingine? Sema ingine basi.

Rael Koech: Karibu na kuwa ya mwisho - ya mwisho ni title deed, mama na mzee waweke sahihi pamoja.

Com. Pastor. Ayonga: Hiyo ndio ya mwisho, ngoja ulizwe swali, na nataka nimpe mama mwenzako nafasi akuulize.

Com. Asiyu: Umesema mama ameenda, amefanya kazi kwa nguvu amepata mali yake, watoto wake peke yake.....

Rael Koech: Wagawe mali ya mama yao.

Com. Asiyu: Kwa maana yule mzee mwingine pengine ameo bibi mwingine, anaweza kuja, ni 'Mrs.' na wewe jina lako pia ni 'Mrs'. Yake. Maana wewe bado hujapata bwana mwingine. Je kama hukupata watoto huko, mali hii yako nani mwingine anaweza kuchukua kama si watoto wa mzee - huyu mzee, inaweza kuenda kwa ndugu yako, kwa mama yako, kwa nani?

Rael Koech: Hapana, mzee atachukua mali.

Com. Pastor. Ayonga: Ngoja kidogo mama.

Com. Zein Abubakar: Mama umesema kwamba katika upigaji wa kura, kuna wanaume wanasema hawawezi kupigia wanawake kura. Na unasema unataka wanawake wawe nao wanachaguliwa kama viongozi. Hawa ndugu zetu Waganda, wametenga viti, wakasema hivi ni wanawake peke yao. Watu wote watawapigia kura lakini mwenye haki ya kusimama, ni mwanamke peke yake, ndio wanawake wakapata fursa ya kuingia bungeni kwa wingi. Sasa sijui wewe unapendekeza bado

wangangane na wanaume? Au wawekewe viti vyao pia wanawake washindane wanawake kwa wanawake, na wapigiwe kura na watu wote, lakini viti watakao simama ni wanawake peke yao.

Rael Koech: Wale wote. Kila mama ako kwa kiti, mzee ako kwa kiti.

Com. Pastor. Ayonga: Mama wa maendeleo nataka ufanye maendeleo kwa kutumia dakika mbili tu.

Lucy Saya: Tuko na memorandum hapa ambayo wakina mama wameandika lakini naona sitamaliza kwa hiyo dakika tatu.

Com. Pastor. Ayonga: Sema majina yako kwanza.

Lucy Saya: Kwa jina ni Lucy Saya. Chairlady maendeleo ya wanawake katika wilaya ya Kericho. Sasa ninataka kusema ya kwamba - kitu cha kwanza, nataka kusema ya kwamba, sisi kama wakina mama, tuko nyuma kidogo kwa mambo ya kisiasa. Vile mama alisema hapa kwamba tunahitaji viti vya mama, tumeonelea ya kwamba tumetembea, tumezunguka kila mahali katika wilaya hii ya Kericho, na mimi ninaona wakina mama wanasema ya kwamba, viti tunahitaji 1/3 katika bunge ya Kenya, kwa ujaguzi huo unakuja. Wakina mama wanauliza namna hiyo. Wanasema sasa hata kama hiyo ya nomination ipewe wamama wawe sawa.

Kazi yoyote kama assistant chief vile mama wamesema, tunahitaji hiyo. Kwa maana sasa nikiona sasa wakina mama wako nyuma. Vile ninaona ni kwamba, pengine kijana anaenda ngambo anapata bibi yake, anakuja na sisi tunaenda kwa uwanja wa ndege tunampokea kama ako na watoto na yule mama mwingine kutoka ngambo. Na sasa kama msichana anaenda huko, pengine anarudi na mtoto peke yake hata akuji na bwana. Tunaulizwa huyu mtoto anatoka wapi, rudisha mali ulikuwa ulete, tunaona hapa kuna shida, kwa maana hawa watoto wote ni sawa. Kwa nini hampokei huyu msichana kama vile kijana tulikuwa tunapokea, tunahitaji hiyo Bwana Commissioners waone hapo, halafu mnaona ya kwamba mtoto kamaa anakuja sisi zote tuko sawa kwa maana tunazaa watoto pamoja.

Kitu kingine tena, tuko na mambo ya mashamba. Ninataka kusema ya kwamba mahali ya mashamba vile tunaona ya kwamba, pengine mzee anaandika hii shamba ni yake peke yake, pengine anachukua loan, hiyo shamba inawezauzwa mara moja, pengine anatoa hii loan bila mama kujua. Kwa maana hata akikuta mwingine anamchukua huko anasena “huyu ni bibi yangu”. Hiyo kazi inaendelea pengine tunashukia tu pengine shamba imewekwa inasemekana hakulipa mambo ya loan. Tunahitaji hiyo title deed iandike bwana, bibi na watoto pamoja. Hilo shamba sitaki liende kwa mtu mmoja. Tunahitaji kama mimi niko nyumba hiyo, hata mimi niko nguvu kidogo.

Com. Pastor. Ayonga: Asante ume-make point yako, kitu ingine?

Lucy Saya: Kitu kingine tena ni mambo ya watoto. Mtu kama anaoa sasa bibi yake, pengine ukikaa kama miaka ishirini hivi, pengine analeta mwingine, ninajua ya kwamba kabila yetu Kipsigis hawawezi tosheka na mama mmoja, hawa wanataka watu wengi. Pengine ninaoa, mimi ninafanya kazi pengine tumenunua duka, mwishowe, kama huyo mama anaingiea pengine anasema hii mali yote - pengine ni bahati mbaya huyo mtu akufe - anasema hii mali yote tutagawa katikati. Lakini tunaona hiyo ni shida, lazima aone kama huyu mzee anaona hakuna kusema wazee hawaoi, hiyo ni desturi yetu. Lakini, kama anaoa kutoka hapo kama kuna mali, awachie huyo mama mkubwa halafu mzee aendelee kutafuta ingine.

Com. Pastor. Ayonga: Hebu tunyamaze tusikie maoni ya mama.

Lucy Saya: Sasa kutafuta hiyo ingine, mali ingine kutoka hapo, aniwachie hiyo, mimi ninachunga nayo watoto lakini sasa ile ingine yeye anamtafutia mali, pamoja na mimi tena. Kwa maana yeye alisema tunaweza hao watu, lakini shida yetu wamana ni kuona sasa ameo, amekuja kukata hiyo mali yangu na huyo mzee pengine kazi yake imekwisha amekuja retire, anakuja kuo halafu anatupatia umasikini ndani ya nyumba.

Com. Pastor. Ayonga: Ya mwisho.

Lucy Saya: Ya mwisho, ninataka kuwaambia kina mama, sasa hizi viti tunauliza kama Concillors, wakina mama waone kama wenu wamesimama, muunge mkono na kuomba wanaume wawapigie kura. Ndio hiyo.

Com. Pastor. Ayonga: Asante lakini kuna swali. Swali unaulizwa na mama mwenzako kwanza, ndipo nitakuuliza swali.

Com. Asiyu: Umesema kwamba wanaume wanapenda kuo bibi wengine, na hiyo unasema iendelee, lakini unajua kuna nchi jirani kama Tanzania wamekataa, polygamy na iko kwa sheria ya kwamba bwana awezi kuo bibi wa pili, hebu ni malize, isipokuwa iwe na sababu kabisa. Hapa Kenya tulisema, saa zile msichana akiolewa, bwana amuambie kwamba kwa uoji huu katikati yangu na wewe uwe potentially polygamous yaani siku ingine mimi ninaweze kufikiria na nikaleta bibi mwingine. Au aseme sitaleta bibi mwingine kwa hii sheria mbili, hivi unaona inaweza kufaa watu wa Kenya. Hapana Kipsigis peke yake.

Lucy Saya: Unajua sasa nikiongea hapa, ninaongea kwa maana mimi ninajua mila ya Kipsigis zaidi, mimi sijui mali pengine, na sasa unajua pengine kama mtoto wako anaoa, na bibi huyo wa mtoto wako hakuzaa watoto, ama pengine unajua kabila yetu sasa, wengine tena ninaona wanazaa wasichana wanasema hapana, wanaeza kwa sababu hiyo, lakini kitu mbaya sasa ni kuona mtoto wako kama pengine hakuzaa watoto, ninakubaliana hapo, aoe halafu apate watoto. Upendo wa watu ni watoto.

Com. Asiyu: Hayo nimesikia nimekubali, swali la mwisho ni hili: umesema mali iandikwe kawa jina la baba na mama, na ukaeleza kwamba saa zingine baba anaweza kwenda town akapata msichana akapeleka kusema huyu ndiye bibi yangu wanaandikiana halafu wanasema hiyo mali ni yao. Na hata hiyo kama mtu ana akili mbaya namna hiyo anaweza kuchukua watoto wengine wawili hapo chokora town, abebe na huyu mama waseme hawa pia ni watoto wao, na wewe hujui kama

mambo hii imefanyika. Je, ungependa majina yote ya huyu mama na huyu mzee iandikwe ili yule mama mwingine akienda kule ikute jina yako sio yako?

Lucy Saya: Hana kipande, kipande ndio inaongea kwa maana tunaliza jina ya mzee yangu inaandikwa yote, sasa ikienda hata ikikosa hawa watoto haiwezi kosa yangu.

Com. Asiyu: Hiyo sawa. Asante sana.

Com. Pastor. Ayonga: Mama sasa uende kule ujiandikishe na asante kwa maoni yako. Tumefunga kikao cha wamama na maendeleo ya wanawake. Sasa tunataka maendeleo ya wamaume. Peter Chepkwony, halafu kutafuata Peter na Pastor Johah Keino, Pastor uwe karibu, Chepkwony dakika ni mbili. Karibu tutaanza kuingilia dakika moja na nusu. Unamaandishi hatutaki utusomee, tuambie yale yaliyomo tu.

Peter Chepkwony: Sawa sawa asante sana. Yale ambayo ninayo hapa, ni mambo makuu ambayo yametolewa na kanisa katholiki la Chepsiolo. Jambo la kwanza, sitasoma mengi, ni kuhusu wabunge ambao wamechaguliwa, ikiwa kama mbunge hatatekeleza kazi ama wajibu, kuandikwe kutokuwa na imani kwake katika muda wa miaka miwili, ili wananchi wapige kura ya kutokuwa na imani kwake ili atolewe. Vote of no confidence.

Ya pili, wabunge maalum na madiwani maalum, wasiwekwe kwenye katiba kwa sababu hawana kazi maalum kwa wananchi. Ya tatu, kama kutakuwa na masaa ambayo wananchi wanatoa kwa kama ni mashirika mbali mbali, malipo haya yapatiwe kwa muda wa mwezi mmoja. Kama malipo haya yatachelewa, walipe pamoja na interest. Halafu kusuluhisha mambo ya kuwa na njia katika nchi ya Kenya, wakulima wapewe soft loan ili wapate kuendeleza kilimo yao. Halafu kama wamepata mazao wapate ku-make marketing board ambayo itauza mazao yao, na hiyo marketing board wale madirectors ambao watachaguliwa na wakulima wenyewe. Ni hayo tu asante.

Com. Pastor. Ayonga: Asante sana. Pastor Jonah Keino. Dakika mbili.

Pastor Jonah Keino: I am Pastor Jonah Keino from Chepcheliot sublocation in Kipkelion division. Pentacostal church. My views on basic rights. The Constitution of Kenya, should guarantee freedom of worship which should be like this; they should be allowed to register all churches, because the current Constitution does not fully serve because sometimes you may be told from up there, after passing through all the security formalities, in registration of churches, whenever it reaches up there, someone there on reason known to himself may nullify your registration. So, it needs all worship crue should be given to worship regardless of any. Moreover they will be governed by security loss of the land, that is basic rights.

Second system of the government; we should adopt a parliamentary system of government in which a prime minister is

appointed from the majority part in Parliament and the President should be ceremonial only and should be elected by Parliament from the citizens who are qualified. The prime minister should be the head of the government and should elect this cabinet from qualified citizens of this country.

Legislature; Parliament should have unlimited power to control its own procedure through standing orders. Parliamentary candidate should be people of good moral values and integrity with a questionable character.

Age limit for voting, should be not less than 18 years. Contesting of Parliament should be not less than 45 years and not more than 80 years. Parliament should have power to remove the executive through vote of no confidence. The Constitution should regulate formation management and conduct of political parties. The number of political parties should be limited to reflect the national out view because the current formation of political parties only reflect tribal out look, so they should be limited to three political parties and they should be financed through the consolidated fund by setting a commission of enquiries to set terms and conditions of financing that.

Com. Pastor. Ayonga: Thank you very much. Ngoja kidogo. Unasema, kwamba registration ya makanisa kwamba watu waruhusiwe kufanya registration bila masharti, kwa maana umeenda huko au makanisa yameenda huko kwa registration, na wakielekea kule juu, registration inakuwa nullified. Na, umetaka kutuambia kwamba, ikiwa Registra of societies anaweza kuona mambo fulani Fulani - kwa maana anajua kanisa linakuwa registrered kwanza lazima litoe Constitution yao, na kama Constitution hii itaonekana(inaudible) not in Kenya. Au unataka aje?

Pastor Jonah Keino: Imekuwa hivi. After presenting the constitution of that church, it has to pass through the security formalities from the grassroots, that is what is happening now. After passing - after they give you a clean bill of health, there is only one person, mtu mmoja tu anasema hapana.

Com. Pastor. Ayonga: Mtu mmoja si committee?

Pastor Jonah Keino: I've passed through that situation.

Com. Pastor. Ayonga: Kwa hivyo, kanisa lako lilinyimwa registration, is that what you saying.

Pastor Jonah Keino: Yes.

Com. Pastor. Ayonga: Okay. Thank you. Toa makaratasi yako – Pastor, makaratasi yako kule na ujiandikishe.

Com. Pastor. Ayonga: William Magori, sasa karibu tuende dakika moja na nusu. William anapojitayarisha, Hillary Cheruiyot

yuko? Hillary yuko wapi? Uje hapa karibu. Dakika moja na nusu.

William Magori: I am William Magori. From Taragon I here on behalf of Pondene self group and help group. Let me say as written. The views written here is that, tuwe na muundo wa serikali ambayo inayounganisha wanasiasa wote. Secondly, mwenye atakayeshinda kura ya Uraisi, ni sharti awe na kura nyingi pamoja na viti vingi vya ubunge katika bunge. Pia afaulu kwa kuwa mbunge kutoka eneo lake. Tatu, mwenye atakayeshinda uraisi sharti awe na kiwango cha asilimia za kura ishirini na tano katika mikoa tano. Ya nne, Mkenya ana haki ya kurithi ardhi na mahali pahali popote nchini. Halafu ingine, walemavu wa kila aina sharti wawe na budgeti yao ya kuwalinda katika budgeti ya pesa za serikali. Halafu ingine ya mwisho, mamlaka ya uraisi sharti ipunguzwe na bunge iwe na uwezo wa kuteua mkuu wa majeshi, mkuu wa polisi, mkuu wa sheria, judge mkuu, pamoja na Macommissioner wengine.

Com. Pastor. Ayonga: Asante sana. Uende huko utupe hiyo karatasi. Next ni Hillary, dakika moja na nusu.

Hillary Cheruiyot: Good afternoon to you all. My names are Hillary Cheruiyot from Kinugu location. Much has been said but I want to emphasize a few. First the President who is in power, should not campaign for any society or any party, therefore, he should be neutral.

A Member of Parliament should have head office in the centre of his constituency.

The party that is in power should have the responsibility of ensuring that all Kenyans should enjoy basic rights such as education and health.

Mayor and chairmen to be elected directly by the people.

The last is that the President or the local authority and the MPs candidates should be law abiding citizens, without any criminal records and can be able to a law his or her region to be infected before coming to power. Thank you.

Com. Pastor. Ayonga: Thank you so much uende kule ujiandikishe, pande hii, Joseph Cheruiyot anapokuja Joseph Langat awe karibu. Dakika moja na nusu.

Joseph Cheruiyot: Kwa majina yangu ni Joseph Cheruiyot kutoka Lemosit location, tarafa ya Londiani. Ninapenda kusema machache ingawaje mengi yamesemwa sitarudia. Yangu nitaongea juu ya utamaduni. Katiba yetu ihifadhi utamaduni wetu wa kila kabila kutoka nchi hii ya Kenya. Kwa sababu ikiwa kuna jambo, utamaduni ama mambo ya desturi au mila za watu wanajua namna ya kutekeleza wajibu wa watu wao. Jambo lingine ni kuhusu siku ya kuabudu, siku ya Sabato iwekwe katika Katiba ili watu wanaopumzika siku hiyo, wawe huru wa kuomba na hata kwa makazi mahali wanafanyia kazi wapewe

kupumzika. Kuhusu misitu, misitu iwe chini ya county council. Mashamba yote mengine yawe chini ya county council. Kama plots, tusije tukapata ama kuona Commissioner of lands anapeana shamba kule juu, na watu wenye mashamba hawajui shamba hilo lilienda lini, so ni heri iwe chini ya county council.

Corruption; corruption unit ianzishwe katika wilaya. Ili ianze kuangalia hiyo kazi na ifanye kazi kama idara ingine. Corruption iweze kuondolewa na watakaohusika.

Uongozi; ningependa kusema mtu kama village elder, naye alipwe kitu, machief na ma assistant chiefs wachaguliwe na wananchi. Jambo lingine nikienda kumaliza ni kwamba trespass katika nchi hii ya Kenya, iliondolewa zamani, na tuweke Katiba ya kwamba, movement iwe rahisi kwa kila mtu mahali popote atembeapo. Trespass isije ikaonekana.

Mimea ama vitu ambazo tunakuza mashambani, ikiwa ni mingi mahali fulani, factory iwekwe huko, isije ikasongeshwa na kusema headquarters ni mbali, na mahali mimea hii inatokea.

Investors ambao watakuja nchi hii, mali yao wanapopata mali yao, wawe free kuwa na mali yao, lakini 50% ya pesa hizo ziwe za nchi hii. Ili serikali iweze kuwa na venue ya kuendesha kazi. La mwisho, umbrella ya kitu yote, ni lazima tuwe na majimbo ambayo itafunika na kuona kila jimbo na watu wake wanaendelea namna gani. Majimbo ni ya maana na itasaidia kila sehemu kukua kimaendeleo, kimasomo na hata kimaisha.

Com. Pastor. Ayonga: Asante sana mzee kuna swali. Ngoja kidogo.

Com. Zein Abubakar: Unapendekeza sheria kuhusu trespass iondolewe unasema Mkenya awe na haki ya kuenda mahali popote anapotaka. Kama wewe unashamba lako, mimi niwe na haki ya kuingia kwenye shamba lako vile ninataka.

Joseph Cheruiyot: Kuna njia ambayo nimetengeneza kama ni kuingia kidogo ya mguu, kuna mahali imetengenezwa mtu anaruka na anapita.

Com. Zein Abubakar: Wewe unatengeneza njia ya kupita shamba lakini - yaani wewe ndio unatengeneza, lakini ukisha nipa mimi haki nitembee kwa shamba lako, naweza nisipende njia hiyo nipite vile ninapenda mimi.

Joseph Cheruiyot: Hiyo ni kuharibu, mtu mzuri, mtu mwenye muhathilibu mzuri, anapita mahali ambapo inaonekana hapa ni njia - ninasema kwa mfano - unaweza patikana ukipita railway, unaambiwa hapa ni hatari hiyo ni kweli na hata tusikie sheria zake, lakini mbona tusitengenezee mahali pa kupita kwa urahisi?

Com. Zein Abubakar: Sasa hayo ni maoni mawili tofauti ndugu yangu. Two different things.

Com. Pastor. Ayonga: Mzee, unajua kama kuna hatari huko kwa kupita kwa railway, hatari ni hatari, lazima tu-recognize kitu kikisemwa hii ni hatari ni hatari. Kitu ni kwamba, watupatie pahali pa kupita.

Com. Zein Abubakar: Kwenya mashamba kuwe na njia ya kupita watu?

Com. Pastor. Ayonga: Ndio. Mtu hawezi kupita pahali popote katika shamba lako. Lazima pahali paonekane ambako pengine udongo sio mzuri ndio unafanya njia. Thank you so much. Next ni Joseph Langat. Langat uko karibu, mzee uanze kusoma majina yako na uendele. Kimagut John awe karibu.

Joseph Kiptanui Langat: Kwa jina mimi ninaitwa Joseph Kiptanui Langat. Ninatoka Parament, Londian division, Kipkelion constituency. Langu sitachukua muda mrefu kwa sababu tumeandika memorandum.

Com. Pastor. Ayonga: Utuambie maneno tu machache juu ya memorandum.

Joseph Kiptanui Langat: Ndio ninataka kusema machache kuhusu memorandum. Labda nitaomba tu nyinyi Commissioners kwa sababu tumeandika kupitia ule muongozo wa maswali. Hii memorandum yetu mtakapopata mahali imeandikwa no or yes ni kulingana na ile namba tulifuatilia kwa ule mwongozo. Kwa hivyo, letu ambalo tulizungumzia sana ni kuhusu mambo ya majimbo. Na ninasema hiyo kwa sababu tunasikia watu wengine wanakataa serikali ya majimbo bila sababu.

Com. Pastor. Ayonga: Bwana Langat, ngoja kidogo, wazo ambalo umetoa ni kwamba, unataka serikali ya majimbo, hiyo point is well taken, hatutaki kusikia kwa nini wengine wanasema hivi na vile. Asante endelea.

Joseph Kiptanui Langat: Ingingine ni point kuhusu uchaguzi, hii mambo ya uchaguzi, watu wengine wanasema, kura imeibiwa imefanywa nini, tunapendekeza ya kwamba, uchaguzi wakati wa kura inapigwa ihesabiwe pale pale na itangazwe pale ili mambo ya reject isipatikane.

Com. Asiyu: Hiyo tayari imewekwa kwa item.

Joseph Kiptanui Langat: Okay hiyo ni sawasawa. Ingingine ni kuhusu mambo ya umilikaji wa land. Mambo ya mashamba iko na tabu Kenya hii. mashamba tayari yameanza kuwa kidogo, na ingine hakuna hata kidogo. Hakuna haja mtu mmoja awe na maeka elifu kumi, ishirini na majirani wake hawana hata nusu eka. Niliona ya kwamba kuwe na maximum acreage ya mtu. Halafu yule ambaye hana, serikali ipewe uwezo inunue hiyo shamba igawanyie wale ambao hawana, na wapewe kwa njia ya loan na walipe, ili tusiwe na landless Kenya hii.

Com. Pastor. Ayonga: Asante na ya mwisho.

Joseph Kiptanui Langat: Ya mwisho ni kuhusu mambo ya kilimo, area hii Kipkelion tunategemea mambo ya kilimo sana, na tulipoambiwa mambo ya soko huru tulifikiri itakuja kutusaidia. Sasa imekuja kutuumiza area hii, tunataka hii farmer's union,(inaudible) na vyama ambao vinahusika na wakulima waingizwe kwa kikatiba na wapewe nguvu zaidi ili kututetea, yale ambayo tuna produce katika area hii hakuna aja ya ku-import kutoka kwa nchi zingine nje na tumize na tuwe masikini.

Com. Pastor. Ayonga: Asante sana Mzee, ngoja kuna swali.

Com. Zein Abubakar: Hivi sasa serikali ya Kenya, tayari imeingia mikataba na mashirika mbali mbali pamoja na nchi za nje, ambayo yanatulazimisha sisi tuwe na hilo jambo ulilotaja la soko huru, lakini nchi zingine zinafanya hivi; Zinawapatia wakulima mbegu bure, zinawapa pesa za kulima, halafu bidhaa zao zinakuwa bei rahisi. Kwa hivyo hata kama mtu anataka kuleta mazao yake ya nje hawezi kushindana na mazao ya Kenya sababu ya Kenya itakuwa rahisi, kwa sababu serikali inatoa subsidies. Sijui msimamo wako utakuwa nini mzee wangu?

Joseph Kiptanui Langat: Msimamo wangu na wetu hapa kama wakulima ni ya kwamba, sisi tumepoteza mambo ya maziwa yetu inapotea hapa, na kila kitu inapotea kwa sababu ya soko huru ya watu wengine wa nje na tuko nayo hapa.

Com. Pastor. Ayonga: Lakini – asante - sasa Mzee unaweza kuenda kule ujiandikishe. Nilimuita Kimagut. John Kimagut, unamaandishi na nina watu mia moja na kitu wanaoningojea, ninataka tu utumie dakika moja na nusu.

John Kimagut: Kwa maana umenipatia dakika moja na nusu, nafikiri ni vizuri tu kwa maana utasoma hizi zote ambazo nimeandika ni mingi kweli. ningependa tu kusema moja ambayo ninaona mpaka saa hii hatujaanza kusema. Ningependa tu hii maneno ya registered parties, registered union, kama ingekuwa covered kwa Constitution, wawe wakifanya election kwa secret ballot. Kumekuja siku hizi mvurugano kubwa sana unapata watu wanaenda wanafanya mlolongo, this public manner of voting. Imeanza kuwa mingi sana mpaka unaona hata watu kwa nchi wameanza kuvurugana kwa sababu ya huyu mwingine alikaa kwa laini ya fulani, kama registered union, registered parties yote iwe covered kwa Constitution, wawe wakifanya kwa secret ballot all voting system hata kwa general election, hii maneno ya parties ya nomination kama inaweza kuwa covered iwe ikifanywa kwa secret ballot, itakuwa mzuri haiwezi kuleta chuki kati ya watu. Mpaka hapo Bwana Commissioner, afadhali nikomee hapo kwa maana you will have time to read my recommendation.

Com. Pastor. Ayonga: Thank you. Tunataka watu wanaotusaidia namna hiyo, huyu Samuel Busienei, si alikwisha ongea, hajaongea labda ni Busienei mwingine.

Samuel Busienei: Bwana Commissioner, yangu ningetoa tu maoni mambo ya mjumbe ambaye tunachagua katika...

Com. Pastor. Ayonga: Sema majina yako kwanza.

Samuel Busienei: Mimi ninaitwa Samuel Busienei kutoka Rigawa. So mimi ninaongea kuhusu maoni ya mjumbe ama Councillor. Kwa sababu wote wanafanya kazi moja, moja ndio yuko katika council na mwingine ni mjumbe ambaye wananchi wanamchagua kutoka constituency yake. Ninaonelea ya kwamba mjumbe anaenda miaka mitano, na baaba ya miaka mitano, kukaribia mwana wa nne, anaanza kukuja nyumbani, kwa hivyo ningeuliza Commissioner, sijui inaweza kufikiriwa.....

Com. Pastor. Ayonga: Ni wewe unafikiri sio sisi.

Samuel Busienei: Mimi ninafikiria iwekwe wakati mtu ameshindwa kutumikia watu wake, pengine tungekata a fee yeye aondolewe kwa sababu tulimchagua kufanya kazi yake.

Com. Pastor. Ayonga: Sawa umesema hiyo ni point moja, ya pili?

Samuel Busienei: Ya pili, pia wana Councillor katika area yake, baada ya watu kumchagua na kusema nitafanya ile, baadaye anakaa miaka mitano akatoka bila kufanya chochote lazima akatwe a fee yeye aondolewe mwingine aingie hata miaka tano.

Com. Pastor. Ayonga: Sawa sawa, ya tatu?

Samuel Busienei: Ya tatu, ninasema asante.

Com. Pastor. Ayonga: Okay sasa Mzee enda kule ujiandikishe. Haji Hussein Omari, halafu kuna John Sigei, Haji Omari, hebu, una dakika moja na nusu endelea.

Haji Hussein: Mimi ninaunga huyu sasa anatoka.

Com. Pastor. Ayonga: Sema majina.

Haji Hussein: Haji Hussein Omari. Huyu anaondoka sasa ndiye mimi ninaunga kidogo ninaongeza chumvi kidogo. Kwa maana Mbunge sisi tumechagua, Mbunge tulipomchagua, badala kuja kutumikia mahali alipochaguliwa, Mbunge anakwenda miaka tano Nairobi. Na alichukuliwa hapa Kipkelion. Macouncillors vile vile nguvu yao lazima iwe anashirikiana na Mbunge na mbunge hata akanyagi hapa, je Councillor watafanya kazi yao namna gani? Wewe mwenyewe ndio unapita barabara hii, hii barabara wewe unaona na macho yako. Kutoka Kipkelion, “Kakarabakarukaru” mpaka lini? Haenda hata Kisumu, kufika hapa hakuna pahali wewe utapita uongo mbaya. Ya pili,

Com. Pastor. Ayonga: Wewe unataka aje?

Haji Hussein: Ya mwisho, hii sheria sasa mnatunga muweke katika sheria kuwa Wabunge wasiwe Nairobi, wawe na watu wa hapa, wajengee ofisi hapa, watumikie na watu hapa.

Com. Pastor. Ayonga: Kwa hivyo mzee unataka wakae hapa?

Haji Hussein: Iwekwe kwanza kwa orodha ya sheria, wakae hapa wanalie pahali walipochaguliwa, wajenge nchi.

Com. Pastor. Ayonga: Okay asante sana Mzee Hussein Haji. Sasa uende kule mzee ujiandikishe, umeweka chumvi ya kutosha. John Sigei, una dakika moja na nusu tu.

John Sigei: Maneno yangu ni machache tu, mengi yamesemwa na watu ambao wamekuja hapa. Lakini langu ni, tukiwa kama tunataka kuhifadhi culture, vitu vingine tuliletewa na Wazungu. Kama ukitaka kuoia, unapata certificate kwa kanisa, ingine iko kwa D.C. lakini wewe Mwafrika, ukioa kinyumbani, hupati certificate.

Com. Pastor. Ayonga: Kwa hivyo unatakaje?

John Sigei: Nataka kama mtu akioa kinyumbani, apatiwe certificate na chief, kwa sababu ameo kinyumbani.

Com. Pastor. Ayonga: Mzee umefanya point watu wanao oa kinyumbani pia wapate certificate. Point ingine.

John Sigei: Point ingine ni habari ya shamba. Shamba isiwe ya serikali, iwe serikali ya mitaa na mwenyewe. Kwa sababu ikiwa shamba litakuwa la serikali kuu, serikali kuu itagawa vile inataka, lakini ikiwa ni ya county council na mwenyewe, county council na mwenyewe wataona vile watagawa hiyo shamba.

Com. Pastor. Ayonga: Point ingine ya mwisho.

John Sigei: Point ya mwisho ni introduce land tax. Kama ukiwa na shamba elifu tatu, hekari elifu tatu, utoe kodi, usinyanganywe ulinunua. Toa kodi kwa kila eka. La mwisho ni habari ya education na employment. Tukitaka watoto wote waelimike Kenya hii, kutoka form four waende university, tufuate quota system. Vile vile kazi ifuate quota system.

Com. Pastor. Ayonga: Asante hiyo ni point yako ya mwisho ya quota system, university na kwa kazi.

John Sigei: Ya mwisho ni serikali ya majimbo, majimbo kwa sababu tutaweza.....

Com. Pastor. Ayonga: Hiyo tunajua mzee, kile majimbo itafanya, tumejua tayari.

John Sigei: Una swali?

Com. Pastor. Ayonga: Hatuna swali.

John Sigei: Asante.

Audience: (laughter)

Com. Pastor. Ayonga: Tafadhali ujiandikishe na utupe hayo maandishi hapa mzee - fuata kule. Sasa ninataka kusema kitu, msije mkafikiri ninawaharakisha bure. Nataka mtusaidie: kama points ambazo ulikuwa umepanga, mwingine amezisema. Si hayo imetosha? Na tena kuna wale mlio na memorandum, si lazima utusomee memorandum, unaweza kuenda kule nyuma ukatoa memorandum yako. Kwa hivyo hebu tufanye kila mmoja apate nafasi. Ikiwa unajambo ambalo ulitaka kusema na limesemwa, ninapokuita, sema niliyotaka kusema yamesemwa tayari. Ikiwa kuna jambo jipya ambalo halijasemwa, kwa wale ambao mmesikia kutoka asubuhi, basi hilo uje na uliseme. Sasa ninamwita Joseph Too. Una dakika moja Joseph, sema majina yako na endelea.

Joseph Too: My names are Joseph Too from Koroi South. My first point is taxation issue. We want to get rid of this idea where one person have in mind this thing of secret issue. We want to know from the incoming the immediate heir.

The auditing of public funds. Receipts have to be put off. This is because some draft staff have taken advantage of writing some false information.

Parliament must not be given monopoly and autonomy in preparation of budget speeches. I propose that before the day of budget, some committee has to go round collecting and collecting views from the public.

Vesting management committee, to a certain deficiency and efficacy of civil servants.

We should have in Kenya a one man-one job.

Com. Pastor. Ayonga: Asante. Hebu chukua kule na ujiandikishe, pande hii. Josephat Samoe. Ni wewe? Samoe dakika ni yako. Sema majina yako. Usiharibu.

Josephat Samoe: Majina yangu ni Josephat Samoe. Langu tu ni kuunga mkono yale yamesemwa.

Com. Pastor. Ayonga: Wewe ni mtu mzuri sana.

Josephat Samoe: Yangu wenzangu wenye wamezungumza wamesema yale nilikuwa nayo.

Com. Pastor. Ayonga: Asante sana. Tena unaongeza?

Josephat Samoe: Kitu chenye nitaweka mkazo ni serikali ya majimbo, ili tuwe na serikali ambayo itasaidia Wakenya wote. Kwa sababu kuna jamii ambao hawatambuliki Kenya hii, kama Wadorobo, Watalai, lakini tukifanya serikali ya majimbo hawa watu nao watapata kuingia serikali ambayo ni ya kikamilifu.

Com. Pastor. Ayonga: Asante sana. That point umesema tayari, unataka serikali ya majimbo.

Josephat Samoe: La kumalizia ni maneno ya shamba. Tunasikia kuna Commission ya land huko Nairobi. na shamba haliko huko Nairobi, liko Kericho ama mahali pengine. Kwa hivyo mambo yote ije katika Local Authority.

Com. Pastor. Ayonga: Okay asante sana. Sasa uende pande hiyo ujiandikishe.

Josephat Samoe: Niko na moja.

Audience: (laughter)

Josephat Samoe: La kumalizia, ni la kwamba kuna constitutional review, lazima itengenezwe kulingana na culture ya watu, tusije tukakopa kutoka culture za huko ngambo tulete mji huu. Kama hii ya kusema ya kwamba, tugawane mamlaka. Kwa culture yetu, itakuja kuwa vigumu.

Com. Pastor. Ayonga: Asante enda huko ujiandikishe. Stephen Sawe, ana maandishi juu ya kanisa la katholiki, tutapata hayo maandishi. Elisha Kalia, una dakika moja na nusu, utuambie uliyo nayo, yale makubwa tu mengine tutasoma.

Elisha Kalia: Kitu ambacho ningeliomba Bwana Commissioner, ni ya kwamba, hizi memorandum ambazo nilipatiwa na wazee wa Londiani division na hawa wazee wako hapa, pengine wangependa kusikia kama nimepeana kulingana na vile walitoa.

Com. Pastor. Ayonga: La, hatutataka uje kutusomea. Umekuja kutupa kwa nafsi yao kwetu - sisi ndio umeletea,

hukuwaletea, kwa hivyo umulike kama kuna maneno mawili matatu makubwa, tuambie hii na hii. Kama hiyo ndio unataka wasikie.

Elisha Kalia: Okay asante. So I can read it ya kwamba, we people of Kenya, need a preamble in our Constitution.

Com. Pastor. Ayonga: Okey, we need a preamble.

Elisha Kalia: We need this to be recognized by the constitutional makers. This will enable mwananchi to refer, and the agreement reached and retained for the young generation. In most cases the preamble is very important to every Kenyan. For example, we in Kipsigis tribe, have many preambles which were not written e.g. customarily law, which comprises many activities including movable lativals. Therefore, we need all this to be protected and be promoted in the Constitution in terms of customarily law.

Ya pili, hata mimi ninaruka kabisa. It is the structure of the government system, but that one has been said, kwa sababu imesemwa, ya muhimu kabisa kulingana na structure ya government na wale wazee pamoja na mimi tulionelea ya kwamba, a federal system of government be established. Hiyo ndio majimbo. And if it will go through, the name be formed in the name of federal republic of Kenya. That will be the name if it goes through.

Ingingine ambayo imesemwa na marafiki zangu, ni hii mambo ya marriage of culture ya kwamba, tumeonelea ya kwamba kweli certificate of marriage, traditionally be issued and even those certicates from the D.C.s office be centralized in the chief's office. So that the family who are marrying each other, can receive those certificates.

Ya mwisho, are those people who are impregnating the school children. Kama mtu akimweka mimba mtoto wa mtu, ni lazima amuo no matter whether he has got many wives, lazima aoe, otherwise, akikataa kuo, lazima asomeshe huyo mtoto mpaka university na ampeleke college halafu sasa amuachane asipooa mama yake. That is when tumefanya hesabu itaweza kuwa 26 years kuchunga huyo mtoto.

Ya mwisho, ni mambo ya Councillors and the powers of the council. Tulionelea ya kwamba, kwa sababu tunataka nguvu yote iwekwe kwa county council, in order that to be well enough, ni lazima this small other councils, town council and urban council ivunjwe halafu nguvu zote ziwekwe kwa country council. All the resources, all the collection on whatever iwe centralized in the county council to meet the need of the community. Kwa hayo machache, nasema asante I think zingine ambazo niliwacha mtazipitia.

Com. Zein Abubakar: Asante sana Mzee Elisha, uende pale nyuma u-sign memorandum. Sasa wale waliokuja wamechelewa mimi kwa vile nimepata fursa ya kuendeleza kazi hii, wazee wanapumzika kidogo, ninamajina yamefikia mia moja arobaini.

Ningependa tu kurudia kwa kifupi mambo tuliowaeleza wale waliofika mapema kuhusu utoaji wa maoni. Lakini kwanza kabisa ningewaomba hawa wazee wawili waliokaa hapa, make kwenye vile viti vile pale tafadhali. Nyinyi wazee wawili mliokaa hapa mbele, mukae pale kuna viti viwili mukae pale. Na nina sababu nzuri ya kukuomba ufanye hivo mzee wangu. Sasa nitaita majina ya watu sita sita au saba saba waje wakae hapa mbele. Ngoja tunaenda taratibu, badala ya kuita mmoja anajivuta dakika moja au dakika mbili anafika hapa. Nitaita watu saba wakae hapa, kwa laini vile nimeita majina. Mmoja anatoka mwingine anaingia, mmoja anatoka mwingine anaingia, ni sawa hivyo.

La pili, tumesema wale ambao wana written memorandum, kuna njia tatu za kutoa maoni - njia tatu. Ya kwanza ni kwamba, wewe huna maandishi, umeandika maandishi yako vizuri kabisa kila kitu ukusahau umeweka hapo. Ukiwa unataka kuyatoa maandishi hayo bila kuzungumza, usingoje jina lako liitwe, uende pale nyumba utoe maandishi, u-sign register, umemaliza kazi yako. Sawa hivyo? Njia ya pili, wewe una maandishi lakini unataka kuja kugusia yaliyo muhimu peke yake. Unaruhusiwa kuja kugusia maoni muhimu peke yake. Na kwa vile hayo maandishi ama hiyo memorandum utatuachia sisi tuifanyie kazi, unahaja kututajia kila kitu. Uchague yaliyo muhimu peke yake ndio waweze kujua unasema nini, au si sawa hivyo?

Njia ya tatu ni mtu kuja kusema yaliyo moyoni mwake na kichwani mwake, bila maandishi azungumze kwa mdomo. Hiyo pia inakubalika. Lakini kama alivyokuwa akiimiza mzee, useme mara moja umalize, point kwa point kwa point. Sasa mimi nitatoa mwongozo kuhusu kutoa maoni namna hiyo. Kwanza yule atakayekuja hapa kusema ya mwisho na ya mwisho karibu na ya mwisho kabisa, huyo ninampiga red card nasema umemaliza wewe. Au si sawa hivo, ukisema mwisho ni mwisho sawa, si mimi nina kuambia wewe ndio ukiniambia mimi ni mwisho, umalizie hapo. Na mimi nikikwambia sema ya mwisho useme ya mwisho. Au si sawa hivyo.

Ingingine ukija hapa ukianza kumshukuru chairman, umshukuru D.O., ushukuru Macommissioner, time zako zimekwisha ninakwambia keti umepoteza wakati wako kwa kushukuru watu. Si sawa hivyo. Kwa hivyo, ninatak kumuuliza mwalimu Amos Nyamu, wenzako walipoitwa wewe ulikuwa wapi? Mwalimu uko wapi? Amekuachia ripoti kimbiba pale nyuma u-sign utoe, uzungumze on behalf of mwalimu Amos, peleka maandishi yake pale, u-sign kwamba umetoa maandishi ya Bwana Amos, sawa. Sikubali mtu amsomee mwenzake, sijui kama unanielewa, yako ikifika zamu yako sema yako, ya mwalimu Amos peleka kule u-sign saa hizi.

Halafu ile sheria ya kusema hapa ni kama kortini watu wako kimya kabisa imerudi, tena kwa vishindo. Ni sawa hivyo. Wacha nichangamshe watu kidogo, sasa nataka Stanley na tuseme mila na desturi mpya kwa ruhusa yenu nyinyi sio yangu mimi, nitamuita mtu mara mbili, kwa sababu tunatumia kipasa sauti, akiitwa mara mbili asiseme “mimi niko” au asiinue mkono kuja hapa mbele, tutaenda kwa jina linalofuatia, au si sawa hivyo. Stanley Koech, mara ya kwanza, kuja hapa mbele mara moja ukae. Ukae karibu na pale. Wycliff Ngeno Lesang, ufuate, Patrice Lesang, Beatrice Lesang, hayuko, Reuben Cheruyo, asante sana mzee umefanya kazi sawa. Rael Chemtai Koech, nilisema sheria ya kuzungumza nimepiga mzee wangu. Mzee wangu mwenye hilo korti la kijivu nimekuona, sheria inasema tusizungumze hapa afadhali tukae kimya ndio kazi ifanyike haraka.

Asante mzee. Rael Chemtai Koech, ameongea, Earnest Cheruiyot, Bernard Momanyi, Zephania Soi, kuja mzee uje hapa kwenye laini. William Chege, uje karibu mara moja ukae kwenye sofa hapa mbele Eliud mimi ninataka kitu hichi chenye rangi nzuri watu wakae huku mbele. Richard Mutai, au wewe ni muai, box yako ni ngapi mzee?

Speaker: Box yangu ni 1009 Londiani.

Com. Zein Abubakar: Richard E. Tonui, uje mzee karibu, na mtu wa mwisho nitamuita apate kiti pale ni Samsom Tono kina kiti Samson. Ni wewe mzee, uje ukae pale kiti cha pale. Mzee wangu wa kwanza niliyemuita wa kwanza ilikuwa ni Stanley Koech. Bwana Stanley utaje majina yako kwa recordi na utoe pointi mara moja, na mimi ikiwa unakwenda kombo ninakurudisha kwenye laini.

Stanley Koech: Mimi ninaitwa Stanley Koech kutoka upande wa Marau na....

Com. Zein Abubakar: Watu wawe kimya.

Stanley Koech: The first point is that power must be developed, majimbo should be there in use. The next one is about land and natural resources should be managed by the County Council. Public officers, majority should be at the district level and a skeleton at the Head Quarters. Passed treaties should be re-examined either in Coast, Masaai land, even in Kericho district whereby people were moved away from tea bushes, so we need to revisit. Community gain - all which has to do with tea should be dealt and finalized here in Kericho.

Contract; the government should not be in business of selling things or purchasing or constructing. Instead, it should give our contracts to people who are accountable so that we can accuse somebody not the government.

Marriage; as we move to the next century, we require law to be put in place, so that marriage as a way of stabilizing the country, should be streamlined. Nobody should marry below 18 years old.

Land; no non citizen should own land.

Malaria; we should put in place a stage whereby we don't treat the symptoms but we treat the cause, so far we have been buying fansidars and all this.....

Com. Zein Abubakar: Unajua umeenda kwenye hadithi, wewe unataka prevention zaidi, primary care iwe prevention.

Stanley Koech: I wanted to say this; we have tick control in this country, so we need to face mosquito control not malaria.

The last one is our Constitution should allow nominated persons especially women - a third of our MPs and maybe of Councillors should be women and that should be there until such a time we have women.

Com. Zein Abubakar: They can compete in politics equally. Thank you very much Bwana Koech. Nataka Bwana Wycliff Ng'eno, Bwana Koech sign kule register.

Wycliff Ng'eno: Okay Bwana Abubakar nashukuru kwa kunipa hii nafasi. First of all I will want you to give me more time than you have given to this other people because.....

Com. Zein Abubakar: You have already wasted a lot of my time. Wewe Wycliff unaona mwenzako sikumzuia, as long as you are making points mimi sitakuzuia, ikifika dakika tatu nitakutoa mara moja. Lakini ukianza kuni-wastia time, you have wasted one minute of your time and one minute of my time. Sikiza Bwana Ng'eno, for the record, state your name and go straight to the point.

Wycliff Ng'eno: My names are Wycliff Ng'eno, representing the Kaplela cultural youth group. So in the Constitution that we are expecting to have in this country, that is after we have made a good one, we need first of all to have the preamble and the preamble if you give me a chance to read the preamble.....

Com. Asiyu: You should read(inaudible).

Wycliff Ng'eno: Very fine. Kenya is a republic - one and indivisible. A democratic State with a President who is sovereign. The sovereign power emanates on the citizens and the President exercises it in conformity with the provisions of this Constitution. Changes in the sections is; we go to the real Constitution, section 4, there shall be a honorary President. Section 5, substitute F, 25%.....

Com. Zein Abubakar: Just hold on Ng'eno. Nilisema hapo nyuma watu wasizungumze. Yule mwenye kutaka kuzungumza atoke na rafiki yake waende kule chini wazungumze wamalize. You are now wasting everybody's time - mzee wangu, najua unanisaidia lakini I can handle it thank you. I am saying this mnaona time tunapoteza kwa mimi kuzungumza na nyinyi, ni time yenu si time yangu, ni time yetu sisi sote pamoja. Nimemsimamisha Bwana Ng'eno, alikuwa anaendelea vizuri sababu kuna watu wanazungumza. Bwana Ng'eno alikuwa hapa amenyamaza amempa mtu heshima akazungumza vile anavyotaka, hakuingiliwa. Sasa Bwana Ng'eno anazuiwa. Ningeomba nisipate fursa ingine ya kuzungumza namna hii tena, tafadhalini. Bwana Ng'eno.

Wycliff Ng'eno: Okay fine; Section five substitute F, 25% votes from five province should be considered and to majority votes. Sub section four them incase of president becoming vacant, by reason of section five, people should be given a chance to

choose again. Section seven, strict and particular dates of assuming forces by the President, should be put in place as evidence in the Constitution. But section 7 and 3, I can't declare the President has seized to hold the office of profit. Section 7 substitute 4, our President should declare wealth as possible to be allowed to operate business to profit. Subsection 14, there shall be a provision to allow the President to be impeached as in the US. Section 15, there shall be an office of the prime minister who shall be appointed by the President among the MPs who shall be the head of executive. Section 16, office of the ministers shall be established by Parliament who determine the number of ministers, this should be abolished for this commands, dictatorship. Section 22, President shall appoint such number of Secretaries as National Assembly may determine. This will check and balance to minimize conspiracy. Section 23 of the Constitution which is having now executive authority of the government depends on the Prime Minister. Section 26, Attorney General should be nominated from the sitting judges of the High court, and Court of Appeal and be approved by National Assembly. Section 34, it should not be compulsory for one to be nominated by a political party, to allow private candidate and minimize cartailment of the promising candidate.

Com. Zein Abubakar: The last point.

Wycliff Ng'eno: Parliament should not alter any part of the Constitution unless it is given direct permission from the citizens for than we shall need a referendum. After the third stage, the committee stage, they come to the referendum in the villages and then they go to the reporting stage and then it will go on. The last one about the land.

Com. Zein Abubakar: No, no, Bwana Ng'eno listen to me. I negotiated these rules and the people conceded and said "yes conduct this meeting in that fashion". If I break the rule with you, I will have to break the rule with everyone else. Please just hand in the memorandum we will read and process each and every memorandum.

Wycliff Ng'eno: Okay thank you. The youth were saying, there is no way for majimbo.

Com. Zein Abubakar: Asante sana Bwana Ng'eno. You took your time and decide to say whatever you wanted to say, any way.

Zephania Soi: I am Zephania Soi from Kaplaba. Political parties; political parties should be limited into four. And, they should be financed equally by the government. System of government is federal. The Executive; any presidential candidate should have at least a degree from a recognized university. The presidential tenure be ten years. Two terms each of five years. The Local Government, all the mayors and council chairmen must be elected directly by the people. Impeachment of the Councillors and MPs. In the side of MPs there should be a document to be signed by the people of the constituency not more than four hundred, Councillors not more than 100 people.

Basic rights; The Constitution, should provide for compulsory and free education, right from standard one to form four, that is primary and secondary level. Land and property rights: The Local Government authority should have powers and should not be empowered to rule all the land from the owners and occupiers. This is the last one. In the title deeds, men and women - and that is why even husbands and children should be written in the title deeds. Thank you.

Com. Zein Abubakar: Bwana Soi uende pale nyuma ujiandikishe. Unaona, Bwana Soi ametaja point, point point na ameenda vizuri. Taja jina na uendelee Sir.

William Chege: I am Willian Chege. Constitution review proposals. The electoral system and process. The electoral process should be designed in such a way as to increase the participation of women and youth in Parliament and local authority. Out of 12 nominated MPs, 3 should represent the youth and 3 others should represent the women. This will enable issues concerning the two groups to be handled accordingly.

Com. Zein Abubakar: We understand that point go on.

William Chege: We should do away with the rule of 25 representation in at least five provinces for presidential election. From the polling date the time when the Electoral Commission announces the presidential candidate, the nation should be having no President and therefore should be under the hands of the Attorney General. This will minimize the(inaudible).

Com. Zein Abubakar: We understand that.

William Chege: The electorate should have the power to remove their MP as their representative if he is non performing. The President of Kenya should not belong to any political party. Legislature; the Constitution should permit coalition government. Each party should be part of the government by having various posts in the government. The presidential candidate ranks position 2, should become the Vice President. The life of each Parliament, should end at the official time scheduled that is five years. MPs should have offices in their home constituency for them to understand the problems of their people. The President should not be the commander in chief of the armed forces. He should only have one post and must be an MP.

Com. Zein Abubakar: Okay William, two questions quickly: the first one is that you are saying that you want the President not to be the Commander in chief. Who will be the Commander - in chief?

William Chege: We can have a senior military officer taking that post.

Com. Zein Abubakar: The reason why Presidents and head of governments are made into commander in chiefs, is so that God forbid if there was a war, they would be able to act quickly and defend the interests of the country accordingly. And that is

a political decision, that is not a military decision, that is a political decision, but if you give it to a military officer, you are asking that military officer to make both military decisions and political decisions.

William Chege: That is my view. Land and property rights.

Com. Zein Abubakar: Nilikuambia last two points, tutasoma hiyo, Chege tutasoma hiyo, the next person please, u-make sure Chege ume-sign na umepeana tutai process. Ndio bwana.

Eliud Serem: Mimi kwa majina ni Eliud Serem, kutoka Matharma. Yangu ningependa kutoa

Com. Zein Abubakar: Ngoja kidogo Bwana Eliud ninajina lako hapa, ninataka kuwashauri Wakenya. Mpaka sasa mimi ninamajina mia moja arobaini - nimeletewa list ya watu wengine imefika mia na hamsini. Tufunge register mpaka tumalize watu ndio tufungue tena au tuendeleo ku-register? Tuendeleo sawa. Endelea.

Eliud Serem: Yangu ni kwamba.

Com. Zein Abubakar: Taja jina lako vizuri tafadhali.

Eliud Serem: Jina langu ni Eliud Serem kutoka Matharma, uko Barshile. Mimi ninataka kutoa yangu yaliyo moyoni. Ya kwanza, nitaanza na elimu - mambo ya elimu Kenya hii, sheria ipitishwe kama vile Rais alipitisha ya kwamba elimu iwe ya bure. Iwekwe kwa sheria na wafanye follow up. Pili, mambo ya cost sharing kwa hosipitali, iondolewe. Ufisadi unaingilia hapo. La tatu, machief wachaguliwe na wananchi. Inge kama Commissioner wa land, hiyo iwachiwe Councillors wasimamie, the nearest councils kwa kila area. La mwisho, mambo ya kuoja, marriage. Wamama wamataka tuwe sawa, hiyo ni sheria. Maoni yangu ningependa ya kwamba, ikiwa nimeoa na baba amenipatia shamba, hata kwa kina bibi watoe shamba kidogo tukutanishe tuwe sawa.

Com. Zein Abubakar: Asante sana Eliud ulisema hiyo ni ya mwisho, kama mambo yatakuwa ni kugawanyana sawa anasema muanze sawa. Andikisha jina kule, endelea mzee wangu.

Richard Tanui: Kwa jina ninaitwa Richard Tanui, first point,....

Com. Zein Abubakar: Mpeni mzee Tanui nafasi najua mmefurahia ino lakini mpeni nafasi.

Richard Tanui: First point, regional government to be established. Second point, 75% of local resources to be spent on a local area. Third point an office of Ombudsman to be established to make checks and balances on those political personnel and other authorities who may be corrupt. Fourth point, chain of companies, 75% of shares to be given to local community.

Fifth point, local authority to be given powers in implementation of various projects according to the wish of the community. The sixth point, subsistence allowance to be given or paid to jobless people those who have no potential resources to exploit. In this regard, number of stealing and burglaries will be reduced. Alteration of constituencies boundaries, electorate to be informed but not a few people to be final decision makers.

Boundaries of various districts to be maintained no alteration without consultation. Customs of different communities, to be kept and e.g. they have basic rights to keep and own their customary weapon as before as no harm. Unwanted pregnancies to be stopped and those who indulge in such act, should take care of the infant children till maturity.

Com. Zein Abubakar: Ya mwisho mzee wangu.

Richard Tanui: Ya mwisho, abortion should not be allowed at all costs it is not good. Thank you.

Com. Zein Abubakar: Asante sana. Uandikishe kule na utoe hiyo memorandum tutaitumia katika kufanyia kazi zetu mzee wangu.

Sansom Tanui: Jina ni Samson Tanui. Yangu ni kuuliza serikali ndio inachunga watu, kuna watu wengi masikini. Kuna watu wengi na hakuna mashamba, watu wote wanazaa hata masikini ndio wanazaa zaidi.

Interjection (Com. Zein Abubakar): Kwa hivyo unapendekeza nini?

Sansom Tanui: Sasa nataka hii Katiba iweke watu wale hawana mashamba, serikali itafute mashamba halafu iwagawie. Sababu hawa wanapenda hata watoto wao wasome pamoja. Serikali iwapatie shamba na watu watoe pesa zao kidogo kidogo na kununua shamba. Sababu kuna wengine.....

Com. Zein Abubakar: Hiyo nimeelewa tumeandika kuna watu wengine matajiri wana shamba wengine hawana, wale masikini, serikali iwasaidie iwakatie shamba. Jambo lingine.

Sansom Tanui: Inginge kama maploti, hapa Kipkelion, nasikia saa zingine wanagawa watu wa hapa wamesha andika, hata sasa sisi tunaona mashamba wameshagawa kwa wadosi na wengine hawajapata. Na watu wa hapa kutoka zamani, nataka watu wa hapa wapate ploti.

Com. Zein Abubakar: Ikiwa kuna ploti za kugawanya hapa katika mji wowote Kenya, wapewe wale watu wa pale pale.

Sansom Tanui: Wa hapo, kuliko wa mbali wanakuja kunyanganya watu wa hapa. Inginge hawa machief wachaguliwe. Sasa

maneno yangu yametoshia.

Com. Zein Abubakar: Sawa sawa Mzee Tanui. Asante sana. Uende pale nyuma utie kidole kwamba umetoa maoni yako kwa Tume ya Kurekebisha Katiba. Nitaita watu wengine waje hapa mbele wakae. Yohana Chepkony, huko? Ni wewe mzee, njoo ukae hapa mbele mzee. Richard Chepkony, hayuko, huyu ndiye mzee yohana mimi ninaita Richard sas, William Koech, karibu Mzee, Kiplego A. Sang, karibu mzee. Harriet Macharia. Hayuko. Ruth C. Rotich. James Maina, Joshua Cheruiyot, Simon Kosgei, Daudi Lasoi, karibu mzee ukae hapa, emmanuel Abdul Ali, wewe ukae kiti hicho, Ali tuanze na mzee wa kwanza ambaye ni Yohana A. Chepkonyi. Mzee Yohana. Endelea mzee.

Yohana A. Chepkony: Mimi ni Johana Chepkonyi. Naishi hapa Kipkelion, nilizaliwa hapa Kipchingang.

Com. Zein Abubakar: Naomba usongee karibu na hiyo microphone ndio tusikie vizuri.

Yohana A. Chepkony: Mtasikia, shauri ya hii koo hakuna.....

Com. Zein Abubakar: Ukisongea karibu na hiyo mashine tutasikia.

Yohana A. Chepkony: Mimi ni mzaliwa na hapa Kipkelion na kitu kilicho cha kwanza - hata ukiona mimi ni mzee namna hii - wale wanajua mtoni, mtoni haiwezi kulingana. Mimi ni mzaliwa wa hapa Kipkelion na wengine wameponyoka wamekuwa sawasawa - vile unasikia watu wanalia mlilo kilio cha shamba - na kitu tunataka cha kwanza katika Kipkelion hii, crown ya Kipkelion ilikuwa ni eka ngapi? Eka nane kutoka kando na kando halafu nyuma yake sasa, tumeonelea sasa, kwa nini mimi niliishi kwa hiyo crown land na nimeondolewa na tayari imeuziwa mwingine? Kwa nini mimi sikuulizwa, “wewe uko na pesa”, halafu nikae, hiyo kilio ni jambo la kwanza. Sijui hata mmeniweka juu wapi, sijui ni chini wapi.....

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo mzee unasema hivi, hii inaitwa crown land au ardhi ya serikali?

Yohana A. Chepkony: Ardhi ya serikali.

Com. Zein Abubakar: Ikiwa itaganywa, yule yuko pale aende aulizwe yeye kwanza.

Yohana A. Chepkony: Angeulizwa, ndio hizo walikuwa wanauliza.

Com. Zein Abubakar: Sawa mzee wangu.

Yohana A. Chepkony: Sababu tunaona '88 tulichomewa manyumba na mpaka saa hii(inaudible) iko barabara tu katika

area hii.

Com. Zein Abubakar: Sawa, una lingine mzee wangu?

Yohana A. Chepkony: Ya pili ni hii; Kipkelion kwa maendeleo ya sasa, tunataka kama maji inakosa, maji iwekwe kwa tangi ya zamani halafu ijaze mchana wote maji haitakosa kwa town hii, sababu sasa maji hata inakwisha, hebu uliza maji saa hii uone kama utaona maji. Kitu ninataka kwanza maji ijazwe kwa ile tangi ya zamani ile ni store. Halafu ile store ndio itagawa maji kwa area ya town, hakuna hata mchana mmoja tutakosa maji.

Com. Zein Abubakar: Ngoja mimi nikuulize swali mzee wangu. Kuhusu ukosefu wa maji, zamani hapa kulikuwa kuna maji mengi, lakini si hiyo pia ni sababu ya misitu imekatwa hapa?

Yohana A. Chepkony: Hii sio ya misitu. Hii ni maji ile inatolewa tinga inapelekwa kwa tangi, halafu hiyo maji inawekwa kwa tangi. Nafikiria hivyo ni sawa pamoja na kuangaliwa wale watu hawana mashamba. Tutafanya nini?

Com. Zein Abubakar: Haya asante sana Mzee. Tumeenda mahali kwingine - hii mpaka nikuulize mzee - tumeenda mahali kwingine wanasema Wakenya, kwamba, wazee wanapata taabu. Wakifika miaka Fulani, serikali iwaangalie, wewe maoni yako ni nini?

Yohana A. Chepkony: Maoni yangu, kwa sababu sasa serikali haioni itasaidia huyo mzee namna gani sababu amezaa watoto chungu mzima.

Com. Zein Abubakar: Sawa mzee.

Yohana A. Chepkony: Chungu mzima wanaoa wanawake watano.

Com. Zein Abubakar: Uende pale ujiandikishe mzee kwamba umetoa maoni, tumeandika kila kitu.

William Koech: Kwa majina mimi ninaitwa William Koech kutoka pande ya Kedawa, ninasimamia group ingine inaitwa Kendrif, huko Kedawa, tarafa la Londiani. Nimesema jina. Kitu cha kwanza mimi ninataka kusema ya kwamba, kwanza ni majimbo, iletwe kama mwaka ile ingine iliyopita siku tulipata uhuru tulikuwa na majimbo.

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo unataka mipaka ile ya majimbo ya mwaka sitini na tatu irudi.

William Koech: Irudi halafu kazi iwe rahisi kwa watu wetu wa Kenya wote. Na tena culture, najua tukiwa na majimbo culture

yetu itasimama imara kwa sababu saa zingine watu wengine kw nchi zao, imeharibiwa na taabu ya watu wengine.

Com. Zein Abubakar: Sawa mzee unasema kwamba watu wakianza kusimamia watasimamia utamaduni wao.

Willian Koech: Commissioner ya tatu ni employment. Ikiwa hiyo system ya federal imeletwa, employment iende 90% kwa wale watu wa hivyo hiyo region. Ya tatu, local government, ipewe nguvu yote isimamie mali yao katika region zao. Kwa sababu...

Com. Zein Abubakar: Hiyo iko clear kwetu mzee kabisa.

Willian Koech: Hiyo ni clear hapo. Inginge education, mambo ya elimu watoto wetu wapete elimu kutoka primary mpaka secondary bure. Na tena kuenda university iangaliwe na quarter system halafu kila mtu apate haki ya mchanga yao na nchi zao zipate kupata kazi na upate masomo. Asante sana.

Com. Zein Abubakar: Ngojeni kuna swali mzee wangu. Umesema kwamba ikifika wakati tumeweka hiyo system unataka wewe - ikiwa tutaifikiria hiyo system unataka majimbo wewe. Unasema katika majimbo yako asilimia tisini - 90% wakati wa employment wawe watu wa hilo jimbo. Nataka unifafanulie hiyo, maanake nini, maanake watu waliokaa hapo au mtu aliyezaliwa hapo?

Willian Koech: Watu waliozaliwa hapo jimbo lake.

Com. Zein Abubakar: Sawa. Asante sana Mzee uende u-sign pale register kwamba umetoa maoni. Mzee Daudi ndio wewe sio, aa, anayefuata ni Mzee Daudi halafu atafuatiwa na Emmanuel Abdula Ali halafu Bernard Ng'eno. Wewe ni nani mzee.

Speaker: Kiplego Sang.

Com. Zein Abubakar: Basi toa jina Mzee wangu. Kiplego A. Sang.

Kiplego A. Sang: Yangu ni kidogo, kwa hivyo mimi ninasema kidogo. Jina langu ni Kiplego Riyan Sang. Kwa hivi mimi ninasema sijui hawa wa squatter wanafunga njia hii zamani, sababu tumefungiwa sisi tumefungiwa, tutafunguliwa lini. Sababu sisi tuko kwa kifingo.

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo mzee wewe unataka kuweco jina squatter, mali igawanyiwe wananchi, kusiwe kuna mtu anaitwa squatter.

Kiplego A. Sang: Zinaitwa sasa sababu mimi sina shamba.

Com. Zein Abubakar: Lakini unataka hivyo, mambo ya squatter iishe watu wapewe ardhi.

Kiplego A. Sang: Ndio mimi ninaomba muwaambie mkubwa wenu wowote yule anaweza asaidie, tena si mimi peke yangu, iko siku moja watu kidogo kama arobaini na sita walichukuliwa kutoka hapa, wale waliofariki, sio wale wako sasa. Na hao waliofariki, wamezaa zaidi kama njugu. Kwa hivyo mimi ninalilia watu hao wote sio mimi peke yangu. Hata wale mimi nimezaa wanapita ishirini.

Com. Zein Abubakar: Hiyo peke yake, enda uandikishe jina kuwa umetoa maoni mzee wangu. Hata kama umekaa Mzee Daudi ni tum yako.

Daudi Latoi: Bwana Mtaa ndio unasikia au unasikia, mimi ninasema neno moja kwanza.....

Com. Zein Abubakar: Sema jina lako.

Daudi Latoi: Mimi ninaitwa Daudi Latoi. Mimi ni mzee wa upande wa Kipkelion kwa mashamba makesi ya mashamba, Kericho. Kuna neno moja ndugu yetu, imeshinda sisi dunia hii, kila mtu sasa hana haya, hakuna haya kwa wakubwa hakuna haya kwa watoto. Hakuna haya kwa kila kitu. Hii ni mambo gani sasa? Mimi ninaona hii mambo, wakati watoto wanaanza shule, si kuna watoto wa secondary saa ingine wanachoma, wanapiga madirisha wanavunja, wanaharibu vitu kwa mashule, kufika university ninasikia wanapiga watu na mawe kwa barabara, hii tabia gani sasa watu wa Kenya namna hii?

Com. Zein Abubakar: Unatakaje mzee?

Daudi Latoi: Sasa, mimi ninataka serikali ianze kuwachunga. Kwa kuwa kuchunga watoto kwa uwanja, watoto wa primary, mwalimu anatakikana awaangalie sawasawa, kwa maana hawa watu hawajui mtu mkubwa.

Com. Zein Abubakar: Lakini mzee sasa, imekuja sheria mpya, mtoto shuleni hufai kumchapa.

Daudi Latoi: Inatakikana watoto wote wachungwe kutoka nyumbani hata kwa baba yao, sababu sasa, wanazaa kusema watoto kwa maana watoto sasa watu wengine wanaogopa mtoto. Eti wanasema wameshasoma. Angalia yale matawi ya miti ile iko juu. Wanasema matawi yameangalia mbali, na huu mti umesimama chini, nani anashika ile tawi. Na ile tawi maana yake ni nini? Kama pepo inakuja si inaangusha?

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo mzee unataka zile heshima za zamani watu wazitumie?

Daudi Latoi: Nataka hii heshima ya zamani iingie kwetu. Kitu moja tena mimi ninaongeza, kusema kila mtu ulikuwa na ikiwa sisi tuliimba zamani - wacha mimi ninajaribu moja. *“Mourenen emenyon, ingen age tugul korenyin”*. Tulikuwa tunasema namna hiyo, hii ni nyimbo ya zamani.

Com. Zein Abubakar: Kwani mzee, sasa mimi nataka uniambie inasema nini. Ngoja mzee aniambie hiyo nyimbo inasema nini.

Daudi Latoi: Tunasema, hiyo nyimbo inasema usicheze na ya mtu mwingine, kila mtu anajua kwake. Basi mimi ninasema hii maneno ndugu yangu inatushinda sisi. Wakati wa uchaguzi unakuja, sababu uchaguzi ni wa binadamu. Nataka kuchagua watu, kuchagua wanasema huyu ninataka kumchagua, nataka kufanya kazi ya Bunge, ya Council au ya nini - hii pesa inatumiwa watu ndio inaharibu dunia hii. Watu wakutumia pesa ndio kitu inaharibu hata kwangu.

Com. Zein Abubakar: Sasa mzee hutaki watu wachaguliwe kwa sababu ya kupeana pesa, wachaguliwe kwa sababu wana mambo mazuri.

Daudi Latoi: Basi, hata hao watu wazee wanakaa vijiji wao kila wakati wanasema sisi tutachagua mtoto wa nani, atakwenda Bunge, nani atakwenda - angalieni sasa watu wanazungumza wasipofika huko unasikia mtoto wa fulani na mtoto wa fulani wanaondoka. Sasa wazee wanazungumza tu hata hawa wazee wanajijua.

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo mzee, unataka tuunge memoranda ya wazee wawe wakikaa chini wakikata shauri.

Daudi Latoi: Hatutaki hawa watu wa nini.....asante sana kuwa hiyo maneno machache lakini inatosha tu wacha.

Com. Zein Abubakar: *“Kongoi missing”*. Asanteni Emmanuel Abdul Ali. Utafuata orodha ndugu yangu.

Emmanuel Abdul: My names are Emmanuel Abdul Ali. Protection of journalists’ press mail. The new Constitution should elect special rules that will protect the journalist - local plus foreigners from the attacks of police, while they are carrying out their official duties. Unaona mara nyingi ya kwamba kunapotokea shida...

Com. Zein Abubakar:.....(inaudible) wewe unataka kunieleze kuhusu the nature of the work of the journalist,(inaudible) lakini wawe protected

Emmanuel Abdul: Wawe protected wasiwe wakipigwa au camera zao zinakuwa confiscated by the government. Freedom of expression; utaona ya kwamba wakati huu, many Kenyans are still being victimized for expressing views that are contrary to the government official version of two. Kwa hivyo tunastahili kuwa na uhuru wa maoni katika Katiba ya sasa. Freedom of

movement; the law should guarantee even citizen the right of movement anywhere he or she feels like. Tumekuwa tukisikia wanasiasa wakipinga mtu na kusema kwamba eneo hili ni langu.

Com. Zein Abubakar:(inaudible)

Emmanuel Abdul: Protection of children rights. The laws on rape defilement section, assault as sexual harassment should be thoroughly reviewed. Why am I saying so, tumeona ya kwamba.....

Com. Zein Abubakar:(inaudible)

Emmanuel Abdul: Plus rape. They should be treated the same. Kwa hivyo mtu ambaye pia amechafua mtoto anastahili kupewa kifungo cha miaka mingi kama yule ambaye ametenda kitendo hicho. Kwa hivyo, hizo sheria zitetee mtoto. Mimi ninapozungumzia children rights, nataka kusema kwamba, mtoto akizaliwa Kenya hata kama ni wa siku moja ama dakika tano baada ya kuzaliwa, basi iwe ni Mwanakenya. Akifanyiwa kitu chochote kibaya, akifanyiwa mathara yote anastahili kuwa anatetewa na sheria ya wakati huu. Judiciary; ni lazima tuwe na supreme court katika Katiba ya wakati huu, yaani korti kuu ambayo itakuwa ikisamiwa na ma judge saba akiwemo judge mkuu plus Chief Justice. The appointment of Chief Justice and high court of appeal judges should be vetted by Parliament first, before the President signs.

The Attorney General office; tumekuwa tukisikia shida moja imetokea hata ma judge wakilalamika hapa nchini Kenya, ambayo inaharibu what is known as miscarriage of justice. The Attorney General has been entering what is known as nolle prosequere. What I mean by this, the termination of a case before it's final conclusion.

Com. Zein Abubakar: I understand what you are talking about, what do you want?

Emmanuel Abdul: I want it to be removed.

Com. Zein Abubakar: So the AG will not have the power to.....

Emmanuel Abdul: To interfere with the case before it is finally concluded by the judge or a magistrate. We have corruption which has become the order of the day in our country. I want now to say how are we going to fight this corruption? In the new Constitution, we should have a permanent and independent strong anticorruption authority, which should have teeth to bite criminals of this nature. It should be headed by a competent qualified criminal lawyer who should be appointed through Parliament. Independent special courts, this number should be established to deal with the sort of corruption cases. The following stiff law should be enacted to deal with corrupt civil servant, this should include sacking them instead of transferring them, confiscation of their ill gotten property by the State, their bank accounts should also be frozen by the State. Give them

heavy jail terms without any fine.

Land issue; the new Constitution should get laws for the acquiring of title deeds for all plots which have been leased for a long period of time by the occupant, for example, 35 to 40 years. Those with “2-TON” should now be given title deeds.

Electoral system and process; voter registration should be made a continuous process. The electoral Commissioner should be appointed through Parliament not by the President. Provincial Administration, the slot of chief. Sublocational chiefs should be done away and all their duties delegated to the office of locational chief. Each village should have a headman, who will be answerable to the locational chief. The locational chief should be directly elected by the people through secret ballot like the first day we used to have it in Kenya. This chiefs should be given very good remuneration or good packages so that they can work and perform their duty very well.

Com. Zein Abubakar: Unayosema itakuwa ya mwisho. Tutasoma hiyo - kila kitu tutasoma.

Emmanuel Abdul: Okay, culture and national language. More effort should be put in place to develop Kiswahili as a national language. We should have a national language governing audio or a national language like we have in Tanzania or Tanganyika.

Com. Zein Abubakar: Asante sana Bwana Emmanuel, tafadhali toa hiyo memorandum. Ameenda mbio mbio, ame-cover mambo mengi. Bwana Bernard Ng’eno, zamu ni yako ndugu yangu.

Bernard Ngeno: Kwa majina ninaitwa Bernard Ng’eno. Yangu nitataja tu machache ingawaje yametajwa lakini bado nitayapitia kidogo,

Com. Zein Abubakar: Unaweza taja na kusema kwamba unaunga mkono au unatilia mkaza.

Bernard Ngeno: Kweli, ya kwanza, ni masquatter wapewe mashamba. Ya pili, ni ufisadi ukabiliwe yaani, upewe adhabu kali kwa yule ambaye atapatikana na ufisadi. Ya tatu, wazee wa mtaa wapewe kitambulisho na pia walipwe pesa kama wanavyo lipa machief. Vyama vya kisiasa viwe peke yake na vibadiliwe na serikali yenye iko kwa mamlaka. Rais achaguliwe hata ingawa yeye sio mbunge apigiwe kura. Ingingine ni ugawaji wa ardhi, tufanye kama vile ilivyokuwa hapo awali. Watoto wa kiume peke yao ndio watapewa jukumu la kurithi ardhi ya wazazi wao lakini, wasichana iwe ni kwa aihari ya mzazi peke yake, akiona kuna msichana mwenye amezaa watoto na pengine ataolewa, apewe shamba. Ingingine ni kuhusu matibabu, matibabu serikali pengine kuna outbreak kama hii ya malaria, sasa serikali ndio itachukua jukumu la kupeana dawa za bure kwa outbreak yenye itatokea. Hata kama ni malaria ama nini, serikali ipewe dawa ya bure. Asante sana.

Com. Zein Abubakar: Unaona Bwana Ng’eno alivyo kwenda, alienda vizuri sikumzuia ameenda ametaja point amemaliza

mara moja. Sasa ninataka kuita watu wengine waje wakae hapa mbele. Samuel Rotich, hayuko, Christopher K. Jeresh. Karibu mzee ukae hapa mbele. Richard Munai, karibu huku Richard, kama uko mbali nikikuita sema niko. James Malel, nimeita Richard Munai sasa ninaita James Malel, naona mvua imeanza kunyesha, kama uko nje kule njoo hapa kwenye kivuli upate fadhila za kivuli hiki. Hayuko James, Wilson Rono, karibu ukae hapa. Stephen Rono, uje ukae hapa mbele, Elija Chepkonyi, karibu mzee, Simon Langat, kaa bwana hapo tafadhali, David N. Tuwei, hayuko, Zigira A. Koech, ameenda, Joseph Kirui, karibu ukae kwenye hicho kiti kidogo hapo. Asante sana. Tuanze na Bwana Christopher K. Cheres. Utaje jina mzee usongee karibu na microphone, songea tu.

Christopher Jeresh: Asante sana Bwana Commissioner wa hii committee. Mimi jina langu ninaitwa Christopher Jeresh kutoka Kimugu location, hii division ya Kipkelion, wilaya ya Kericho. Basi kwa hivyo, jambo langu la kwanza, ni kusema - ya kwanza ninafikiri ya kwamba, kwa kufikiri kwangu, nimesikitika sana kwa hawa watoto ambao wamezaa nyumbani na wamepata mabwana na wamewachana na wengine wameolewa, baada kidogo miaka tatu, miaka nne wamewachana ako na watoto watatu.

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo mzee Jeresh, unatakaje?

Christopher Jeresh: Sasa kwa hivyo kupendekeza kwangu, ni kuuona lazima amri iwekwe kwa huyu bwana ambaye amepata watoto badala ya kurudisha wazazi wao waende wateseke, wazee wa mitaa wafanye kesi na hiyo ni kazi ngumu. Waweke amri ambayo watatii hawa wakae, kama msichana akiwa yeye amekosea bwana, vile vile anataka kifungo ambacho anatosheka halafu akitoka kumaliza kifungu chake bado atarudia bwana yake bado ni mnyama wake, kwa hivyo mimi nafikiri ya kwamba, akiwachilia watu namna hiyo,

Com. Zein Abubakar: Sawa mzee hiyo tumefahamu tumeielewa, ingine.

Christopher Jeresh: Jambo la pili, mimi ninafikiri serikali wakati ambao walipata uhuru, tulipata siku moja na kwa hivyo serikali ni moja hapana kuwa siku moja. Na kwa hivyo mimi ninafikiri hii multiparty ya chama mingi hatupendelei.

Com. Zein Abubakar: Kwa hivyo mzee wewe unataka chama kimoja.

Christopher Jeresh: Chama kimoja kama KANU kimoja. Sababu kiti hii ikinganiwa, hichi kiti(inaudible) sawasawa. Mimi nafikiri tena - a kuongeza hapo, watu wamekuwa wengi sana. Nataka wazee wa mitaa wapate mshahara na hiyo ni sawa. Mimi ninafikiria, Mbunge wakati anaenda bunge, kunatakiwa kupunguzwe mshahara wake, halafu aonekane mwenye kujitolea kusadia wananchi. Sababu, anangangania sisi tumpigie kura aende aketi huko kwa sababu ya mshahara mnono. Mimi ninataka upunguzwe halafu huo mshahara ukuje kwa district ugawiwe wale watu ambao wamesoma wamefanya nini....

Com. Zein Abubakar: Ngoja nikuambie mzee. Kulingana na sheria ya sasa, mtu anaweza kukaa, wakubaliane waniongezee mshahara, wewe unasema uwaambie wao wajiongezee mshara au unataka kuweko sheria ya kuwapunguzia mshahara?

Christopher Jeresh: Sisi tunataka kuweka sheria ya kuwapunguzia mshahara iliaonekane mwenye kutumikia wananchi vile ambavyo waliomba kura.

Com. Zein Abubakar: La mwisho.

Christopher Jeresh: Mimi ninafikiri ya mwisho, itakuwa jambo kama hilo sina lingine.

Com. Zein Abubakar: Asante sana Mzee Christopher, Jeresh uende pale. Mzee Christopher ni mzuri, ingekuwa mtu mwingine angeanza kutafuta kwa kichwa akune kichwa alete ya mwisho ni nini. Endelea mzee wangu.

Richard Munai: Asante sana Bwana Commissioner. Kwa majina ninaitwa Richard Munai. Hii document ya Constitution ambayo tungependelea, tungependelea ihimize zaidi federal government. hiyo ndio federal government inatakikana. Hii Constitution yenyewe ile tulikuwa nayo katika independence haikuwa mbaya. Pengine ni machangilio machache tu wameharibu pale na huko. Kitu tu tungependa ihimizwe ni hii organs tatu, iwe autonomous, na ikiwa autonomous inawekwa nguvu ili ianze kujichek wenyewe. Lingine ni kwamba local authorities, inastahili ipewe irudi kama zamani. Iwe na authority katika mashinani, halafu ndio nguvu itaanza kutoka chini, vile ilivyo sasa nguvu inakuwa kutoka huko juu.

Com. Zein Abubakar: Local Authority kawaida inaendeshwa na pesa hawaganyi na serikali.

